ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
2016 - 2020

1.	**Mhe. Zubeir Ali Maulid**	**-**	**SPIKA**
2.	**Mhe. Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake**
3.	**Mhe. Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni**
4.	**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani**
5.	**Mhe. Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda**
6.	**Mhe. Issa Haji Ussi Gavu**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka**
7.	**Mhe. Haji Omar Kheri**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu**
8.	**Mhe. Haroun Ali Suleiman**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi**
9.	**Mhe. Mohammed Aboud Mohammed**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais**
10.	**Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge**
11.	**Mhe. Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki**
12.	**Mhe. Riziki Pembe Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake**
13.	**Mhe. Balozi Amina Salum Ali**	**-**	**MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais**
14.	**Mhe. Balozi Ali Abeid Karume**	**-**	**MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais**
15.	**Mhe. Rashid Ali Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani**
16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi,**

			Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake
19.	Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
20.	Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais
21.	Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais
22.	Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
23.	Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera
24.	Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni
25.	Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
26.	Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
27.	Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi
28.	Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake
29.	Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
30.	Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake
31.	Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini
32.	Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo
33.	Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo
34.	Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
35.	Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
36.	Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
37.	Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
38.	Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais

39.	**Mhe.**	**Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
40.	**Mhe.**	**Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
41.	**Mhe.**	**Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
42.	**Mhe.**	**Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
43.	**Mhe.**	**Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
44.	**Mhe.**	**Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
45.	**Mhe.**	**Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
46.	**Mhe.**	**Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
47.	**Mhe.**	**Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
48.	**Mhe.**	**Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**
49.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
50.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
51.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
52.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
53.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
54.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
55.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
56.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
57.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
58.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
59.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
61.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
62.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
63.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
64.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
66.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
67.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
68.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
69.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
70.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
71.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
72.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
73.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
74.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
75.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
77.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
78.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
80.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
81.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
82.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
83.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
85.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
86.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

Ndg. Raya Issa Msellem - Katibu

Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 13 Juni, 2018

Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mwanasha Khamis Juma) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 169

Kukamilika kwa Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Ungi

Mhe. Shaib Said Ali (Kny: Mhe. Omar Seif Abeid) – Aliuliza:

Kwa kuwa kwenye sera ya ugatuzi Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ndiyo yenye jukumu la kusimamia vituo vyote vya Afya na kwa sababu kituo cha Afya cha Ungi katika Jimbo la Konde kimeshindikana kutumika kutokana na matatizo ya fedha za kumalizia mambo madogo madogo na kwa sababu Shirika la Posta Tanzania, Wizara ya Fedha (ZNZ), *TBS* na wengineo walishachangia kama walivyoahidi na kwa sababu kazi hiyo imebaki kumalizia shattals za milango kupiga rangi na mabenchi ya kukalia.

(a) Je, ni lini kituo hicho cha Afya kitakamilishwa ili kiweze kutoa huduma iliyokusudiwa.

(b) Je, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo kituo hicho kipo chini yao wamejipanga vipi kuhakikisha kwamba inasaidia ukamilishwaji wa kituo hicho cha Afya.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 169 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Ungi Msuka hadi sasa kiko chini ya dhamana ya Jumuiya ya Maendeleo ya Konde, Jumuiya hiyo ndiyo iliyosimamia shughuli zote zinazohusiana na ujenzi wa jengo hilo.

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni haina uhakika ni nani hasa wamechangia nguvu za wananchi katika ujenzi wa jengo hilo. Lililo dhahiri ni bango la Shirika la Posta Tanzania linalosema ujenzi wa jengo hilo umekamilishwa na shirika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba ujenzi haujakamilika Halmashauri ipo tayari kushirikiana na Wizara ya Afya na Jumuiya ya Maendeleo ya Konde kutafuta namna ya kulishughulikia jengo hilo kwa kuzingatia miongozo ya kisera iliyopo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa mwaka wa fedha 2018/2019 haijatenga fedha kwa kukamilisha ujenzi wa jengo hilo. Hata hivyo bado ipo fursa ya kushirikiana na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Konde pamoja na Mhe. Mbunge kupitia Mifuko ya Kuchochea Maendeleo ya Jimbo la Konde kukamilisha ujenzi wa jengo hilo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ naomba kumuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa vituo hivi sasa wananchi wamejitolewa wenyewe kuvijenga na kusaidiana pamoja na Mifuko mbali mbali ya jamii. Je, Wizara yako inavijuwa ni vituo vingapi mpaka sasa vinavyoendelea kujengwa kwa aina hiyo.

(b) Je, Serikali au Wizara yako ina mpango gani kuvisaidia vituo hivyo ili kuvimaliza ili wananchi wapate kuvitumia. Inshaallah Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Shaib Said Ali swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, uzoefu ni kwamba wananchi kupitia mifuko mbali mbali au kupitia fursa mbali mbali wamekuwa na utaratibu wa kujenga shughuli miradi ya maendeleo ikiwemo vituo vya afya pale popote walipo wanapoona kwamba kuna haja ya kufanya hivyo, pasipo wakati mwengine kuishirikisha serikali kama ambavyo nimejibu jibu hili kwa Kituo hiki cha Ungi Msuka. Hivyo basi ni kwamba wananchi wanajenga baada ya kukamilisha baadhi ya ujenzi au majengo ndio wanakabidhi serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa hivi itakuwa ni vigumu sana Mhe. Shaib Said Ali kwamba kuelewa ni vituo ambavyo vimejengwa kwa njia kama hizi ambazo baadae vitakavidhiwa serikalini. Lakini kuhusu kwa namna ambavyo serikali ipo tayari katika kushirikiana na wananchi katika kuona kwamba dhamira hii inakamilishwa, nimwambie Mhe. Shaib Said Ali kwamba serikali ipo tayari kwa kuwa wananchi wenyewe wameshaona kwamba kuna kero pia, basi na serikali pia haitoacha kuweza kusaidia miradi kama hii ambayo inalengo la kusaidia kutatua kero za wananchi katika maeneo yao popote pale walipo.

Nam. 195

Tatizo la Kushindikana kwa Ufungaji wa Hesabu za Mashirika

Mhe. Shaib Said Ali (Kny: Mhe. Omar Seif Abeid) – Aliuliza:

Kwa kuwa Serikali hupata gawio lake la faida kutoka kwenye mashirika yake kutokana na kutokufungwa kwa hesabu za mashirika kwa kipindi cha Julai/Septemba 2017/2018.

(a) Je, Changamoto gani zilizojitokeza hata kushindikana kufungwa hesabu za mashirika hayo kutoka kwa Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali na kwa kipindi kama hicho Serikali ilipata gawio la kiasi gani kutoka kwa mashirika ya Serikali kwa mwaka 2016/2017.

(b) Je, ni athari gani inayopatikana kutokana na Serikali kukosa kupatiwa gawio lake kutoka kwenye mashirika hayo.

(c) Je, Mfuko Mkuu wa Serikali ulipata mgao wa kiasi gani kutoka Shirika la Bandari, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Shirika la Meli na mgao wa faida kutoka *ZSSF* kuanzia Julai 2017 hadi Januari 2018.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 195 lenye vifungu (a), (b) na (c) kabla naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Utaratibu wa ufungaji wa hesabu za mashirika umeelezwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam. 12 ya 2016 Kifungu cha 110(1)(c) na kifungu cha 121. Vifungu hivyo vinaelekeza kuwa taasisi za umma zinapaswa kufunga hesabu zake na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya miezi mitatu baada ya mwaka wa fedha kumalizika. Mengi ya mashirika yanatumia mwaka wa fedha sawa na mwaka wa fedha unaotumika na Serikali.

Aidha, chini ya Sheria ya Mitaji ya Umma Nam. 4 ya 2002 mashirika yanapaswa kuwasilisha hesabu zake kwa Waziri wa Fedha na Mipango ndani ya miezi sita, yaani robo ya pili baada ya mwaka wa fedha kuisha. Baada ya kupokelewa hesabu hizo, Wizara ndio huwa na uwezo wa kujua ni kiasi gani cha fedha au gawio kinapaswa kulipwa kutoka katika faida iliyopatikana kwa mwaka uliopita kulingana na Sera ya Ulipaji wa Gawio iliyopo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mhe. Omar Seif Abeid lenye vingu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Hakuna changamoto yoyote inayojitokeza katika kufunga hesabu za mashirika. Mashirika yote ya Serikali yanafunga hesabu kwa mujibu wa sheria zinavyoelekeza. Kwa kipindi

cha mwaka wa fedha 2016/2017 jumla ya Shilingi bilioni 1.270 zilikusanywa kutoka katika mashirika ya umma kama gawio la faida.

(b) Iwapo shirika halikupata faida ya kutosha au kushindwa kulipa gawio kwa Serikali, athari inayojitokeza kwa Serikali ni kukosa mchango huo wa mapato katika bajeti yake na hivyo kuathiri matumizi ikiwemo athari kwa huduma za jamii na kazi za maendeleo.

(c) Hadi kufikia Januari, 2018 Mfuko Mkuu wa Serikali ulipokea jumla ya Shilingi milioni 117 kutoka Shirika la Bandari na Shilingi milioni 60 kutoka Shirika la Meli. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii sio mashirika kwa tafsiri ya Sheria ya Mitaji ya Umma na hivyo hayana wajibu wa kuchangia gawio kwani hazikuanzishwa kwa ajili ya kufanya biashara na kutengeneza faida.

Nam. 247

Ujenzi wa Skuli katika Shehia ya Ukutini

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa (Kny: Mhe. Bahati Khamis Kombo) – Aliuliza:

Wananchi wa Shehia ya Ukutini wanaipongeza sana Serikali kwa kuwapelekea maendeleo mbali mbali katika shehia yao. Lakini wao wenyewe walijitolea kujenga skuli ya chekechea wakaendelea skuli ya msingi na Sekondari na walitenga eneo la kujenga skuli ya ghorofa lakini walishindwa kutokana na uwezo wao kuwa mdogo.

(a) Je, Serikali itawasaidia vipi kuwajengea skuli ya ghorofa.

(b) Je, ni lini Serikali italiezeka banda la skuli liliopo katika shehia hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Bahati Khamis Kombo swali lake Nam. 247 lenye vifungu (a) na (b), kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Wizara inawapongeza wananchi wa Ukutini kwa juhudi zao za ujenzi wa madarasa katika skuli yao ambayo yamesaidia sana katika kuongeza upatikanaji wa nafasi za kusomea. Pia nakiri kuwa wananchi wa Ukutini wamejenga jengo la madarasa manne ambalo limeshafikia hatua ya kuezekwa na limeshakabidhiwa kwa Wizara. Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Bahati Khamis Kombo kama hivi ifuatavyo:-

(a) Skuli ya Ukutini ina wanafunzi 967 na vyumba vya kusomea 16. Idadi ya vyumba vya madarasa viliopo vinatosheleza kwa wanafunzi wote kusoma kwa mikondo miwili na baadhi ya vyumba vikabaki. Kutokana na hali hiyo kwa sasa skuli hiyo haina haja ya kujengewa jengo la ghorofa.

(b) Katika mwaka 2018/2019, Wizara itajitahidi kulikamilisha jengo la madarasa manne liliopo baada ya ukamilishaji ujenzi wa madarasa ya skuli ambazo zina mahitaji makubwa sana ya madarasa kutokana na kuwa na wanafunzi wengi kuliko idadi ya madarasa yaliopo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 260

Ukosekanaji wa Hati Miliki za Ardhi kwa Baadhi ya Taasisi na Mamlaka za Serikali

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Katika kuleta mabadiliko ya miundombinu mipya ya kimaendeleo ni busara Wizara na Taasisi za Serikali zinalazimika kwenda sambamba na mabadiliko hayo kwa kasi kubwa. Hata hivyo, baadhi ya Wizara na taasisi hizo zimekwama kuendelea kwa kasi hiyo katika mipango yake kwa kisingizio cha kukosa hatimiliki zinazohusiana na maendeleo ambayo wanataka kuyaendeleza kwa sababu ya kukosekana kwa hati hizo za ardhi na huku malipo yakiwa yameshafanywa.

(a) Je, Serikali inalijua hilo.

(b) Je, ni kweli yapo matatizo hayo au yanayofanana na hayo.

(c) Kama kweli ni sababu zipi zinazocheleweshe utoaji wa hati hizo za Serikali wakati ardhi ni mali ya Serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake Nam. 260 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti**,** Wizara yangu inafahamu kwamba hati za matumizi ya ardhi zilikuwa zikichelewa kutoka.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu imejidhatiti kuhakikisha wananchi na taasisi za Serikali zenye haki ya matumizi ya ardhi zinapatiwa hati zao zenye taarifa muhimu na zenye kuendana na hali halisi ya kidigitali. Katika kuingiza hatimiliki katika mfumo wa kielektroniki, Wizara yangu ilitumia raslimali zake nyingi ikiwemo wafanyakazi wake na kifedha kubadilisha muundo wa hati za matumizi ya ardhi. Kutokana na zoezi la mabadiliko hayo pamoja na hitaji la kuifikisha hati hii katika Serikali Kuu, muda mkubwa ulitumika na kufanya wananchi wengi zikiwemo taasisi za Serikali kuchelewa kupatiwa hati zao. Hivi sasa hatimiliki kadhaa zimeanza kutolewa kwa taasisi zikiwemo Karakana, *ZURA*, Mahakama Kuu na Bandari.

Mhe. Mwenyekiti, kwa suala la malipo ni kawaida ya mwananchi au taasisi yoyote inayoomba kupatiwa hatimiliki kufanya malipo baada ya hatimiliki kukamilika. Hivyo

hakuna malipo ya hatimiliki ambayo yanafanyika kabla ya hati ya mwenye haki ya matumizi ya ardhi kutoka.

(c) Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa taasisi na Wizara za Serikali, hazina pingamizi ya kuendeleza ujenzi katika maeneo yao ambayo hayana mgogoro wowote na yapo chini ya usimamizi wao. Hili hubainishwa wazi wakati Kamisheni ya Ardhi inapojibu barua za taasisi hizi za kuomba hatimiliki hazilipishwi kabla ya hati. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimpe pongezi Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini tuongeze katika jibu la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, tunavyoizungumzia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba ardhi yote ni mali ya serikali na kuna mambo mengi yanayosababisha kwamba vitu vingi vinaweza kuwa vina migogoro kama vile za familia au za mambo mengine ya kurithi na kila kitu, lakini utakuta changamoto nyingi zinatokea katika vyanzo vya serikali ambapo vyengine vipo toka enzi na enzi ikiwemo minara ya kuongozea meli na mambo mengine ambayo yote yanahusu serikali na mambo mengine ambayo yapo yanajitokeza tokeza ili kuvamiwa kwa maeneo yale na kusababisha matatizo mengine.

(a) Je, Mhe. Naibu Waziri atalitatua suala hili la Hatimiliki za serikali ambazo zinaleta matatizo sana na wananchi kuvamia maeneo yao.

(b) Kutokana na mrundikano na sababu ambazo ni za msingi ambazo zinasababishwa na Hatimiliki kuna maeneo mengi ambayo Hatimiliki zake zinakuwa zina hatimiliki mbili mbili. Mhe. Naibu Waziri analizungumziaje hili. Hatimiliki ya kwanza inatolewa na Wizara ta Ardhi. Hatimiliki nyengine inatoka wapi na ina mihuri ya Wizara ya Ardhi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimwambie kwamba uvamizi haukubaliki na naomba tushirikiane kwenye taasisi zote za serikali na wananchi kwa ujumla kwamba tufuateni ile sheria, mtu kilicho chake aseme chake na cha mwenziwe basi akiheshimu. Lakini niseme kwamba lengo hasa la muda mrefu wa kwamba Hatimiliki hazijatoka kama nilivyosema mwanzo ni kwamba tulikuwa tunazifanya bora zaidi kusudi hayo mambo mengine iwe vigumu kufanyika. Kwa mfano kughushi kwa sababu Wizara yangu haitoi nyaraka mbili kwa eneo moja, lakini kama ikitokezea hili basi ni bahati mbaya lakini kikawaida hazitolewi hatimililki mbili kwenye ardhi moja isipokuwa moja itakuwa halali na nyengine itakuwa sio halali. Sasa wale ambao wanatengeneza zile ambazo si halali ndio tunawazuwia katika Hatimiliki hizi mpya.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nachukua fursa hii kwanza kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotujibu, nakiri kwamba wakati umefika tubadilike tuingie kwenye mitandao inayokubalika na tueleweke duniani, lakini pamoja na majibu yake Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati naomba kumuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu yake Mhe. Naibu Waziri amesema hakuna matatizo wamo katika changamoto mbali mbali kuendeleza vizuri. Kwa kuwa Mawizara mbali mbali mfano Wizara ya Elimu ukienda maskuli mbali mbali na ukienda katika sehemu za afya halikadhalika na maeneo mengine ya sekta hizi za wizara. Je, Wizara yake ina mpango gani wa kukaa na Wizara husika juu ya kuondoa matatizo haya kabisa katika maeneo mbali mbali ili kunusuru maeneo yale yasivamiwe na watu wengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba sisi tuna utaratibu huo wa kukaaa na tuna zoezi maalum ambalo tunaendelea na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya kuyapima hayo maeneo na si Wizara ya Elimu tu wizara zote zinakaribishwa kwa ajili ya kuja kufanya utaratibu au kuyapima maeneo yao. Lakini nikumbushe kwamba katika kupima kunakuwa kunaharama ambazo haziwezi kuepukika, hizo ndizo ambazo zingekuwa zinawasilishwa kwa ajili ya kurahisisha huo upimaji. Baada ya hayo nashukuru sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na Mhe. Naibu Waziri kwenye majibu majibu yako umesema naomba kuyanukuu, "Wizara au Serikali hazina pingamizi na kuendeleza ujenzi katika maeneo yao ambayo hayana migogoro wowote yapo chini ya usimamizi wao".

Mhe. Naibu Waziri swali langu lipo hapa. Je, umefanya utafiti gani wa suala hili kujibu hivi maana mimi nina ushahidi wa kutosha, mtu ana hatimiliki ya kumiliki eneo lile ana ripoti ya *EIA* nayo ni ngumu na gharama kubwa sana ya mazingira, ana vibali kutoka *ZIPA* halafu muekezaji huyu leo mwaka wa tatu au wanne anakula hasara na kakopa pesa benki hakuna kinachoendelea. Je, utachukua hatua gani, sitaki kukwambia kujiuzulu utachukua hatua gani nikishakupa uthibitisho huo. Maana yake haya majibu munavyojibu Mhe. Naibu Waziri muwe makini katika majibu ahsante.

Mhe.Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsnte Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjbu Mhe. Jaku Hashim Ayoub wa Paje swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, hakunisikia vizuriri nilisema katika jibu © kwamba upande wa Taasisi na Wizara za Serikali haina pingamizi na kuendeleza ujenzi katika maeneo ambayo hayana mgogoro ambao yapo chini ya usimamizi wao, sikusema kwa mtu binafsi kwa sababu kuna maeneo mengi hasa mfano maskuli yapo ambayo tumesoma na hayana hatimiliki. Sasa yale

ndio ambayo tunayazungumzia kwa Taasisi za Serikali, tunajua *automatically* hapa hili ni eneo la skuli na halina mgogoro kabla ya hatimiliki haijatoka hatuwazui kwenye mambo ya ujenzi.

Lakini upande huu ambao umesema kama kuna watu wawekezaji au wananchi ambao unahisi ni haki yao kupata lakini muda mrefu kwa njia moja nyengine walikwamisha, naomba karibu sana wizarani mlete mtu huyo, lete vielelezo tupate kulitatua tusaidiane na nasema kwa ujumla kwa sasa hatimiliki hazikawii sana hazichelewe, zamani zilikuwa hivyo kwa sababu ya mfumo maalum tumerekebisha mfumo ule kuleta mfumo ulio bora zaidi na sasa umekamilika tayari kwa ajili ya utekelezaji. Ahsante sana.

Nam. 149

Tija ya Meli ya M.V Mapinduzi Ii

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Pamoja na nia na jitihada nzuri ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kununuwa meli mpya ya Mapinduzi II ili kurahisisha mawasiliano baina ya visiwa vyetu lakini meli hiyo imekuwa ikikumbana na maharibiko ya mara kwa mara na lengo kutofikiwa.

Je, ni tija gani au faida imepatikana kwa kipindi chote tokea meli hii ianze kazi.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub wa Jimbo la Paje swali lake Nam. 149 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, meli ni chombo cha usafiri unaotegemewa na nchi yoyote ya visiwa duniani kwa ajili ya mawasiliano na sehemu zinazohusiana nazo au za nchi nyengine. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliponunua meli mpya ya Mapinduzi II ilikuwa na nia hiyo ya kurahisisha mawasiliano baina ya visiwa vyetu lakini pia kutoa huduma kwa wananchi.

Kama kuna tija au faida iliyopatikana tokea meli hii ianze kazi ni, mimi ninasema kwamba faida ipo kwa sababu:-

1. Kuwa na usafiri wa uhakika baina ya visiwa vyetu viwili.

2. Meli ya MV Mapinduzi II ni kubwa na bei ya usafiri ni nafuu na imezingatia hali ya kipato cha mwananchi wa kawaida, kwani ndio ya chini kulinganisha na kampuni za watu binafsi zinazotoa huduma za usafiri wa baharini.

3. Kwa kipindi ambacho meli hii ilifanya kazi kuanzia Januari 2016 mpaka Januari 2018, jumla ya abiria 385,909 wamepata huduma ya usafiri wa meli ya MV. Mapinduzi II ambayo ndio dhamira ya ujenzi wa meli hii.

4. Aidha, safari za Kimataifa zilizofanywa na meli hii, zimeweza kuimarisha mahusiano na kufungua milango kwa sekta nyengine zikiwemo za biashara, utalii, utamaduni na kadhalika, baina ya nchi yetu na visiwa vya Comoro na Kenya.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza niendelee kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa nia yake nzuri sana na historia itamkumbuka na itaendelea kumkumbuka. Ninafikiri katika kumbukumbu zangu ni Marais wawili tu walionunua meli, akiwa ni Mheshimiwa Marehemu Aboud Jumbe Mwinyi aliponunua meli ya MV Mapinduzi, Maendeleo na Ukombozi na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein historia hii itawakumbuka sana Marais hawa, amefanya kitu kikubwa sana na cha kupongezwa.

a) Lakini kutokana na kadhia hii watu wametumia nia mbaya sana na kutusababishia matatizo makubwa sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri, naomba nifute kauli yangu nisije nikakushusha cheo chake chini, nilikuwa nimeshakuzoea Naibu Waziri kutoka Wizara ya Afya, sasa hivi ni Waziri wa wizara moja kubwa sana. Mhe. Mwenyekiti, atakuwa tayari kutupa mualiko kwenda mguu kwa mguu kwenda kuona meli ile kupata ukweli wa hali ilivyo kutualika kwa atakayetaka lakini mimi naomba ku-*declare interest* nipo tayari kwenda utualike twende tukaone hali ilivyo. Na kuna taarifa pesa zilizoingizwa ni nyingi zaidi katika matengenezo yale, hamuoni ipo haja ya kwenda kununua meli nyengine baada ya kutia pesa mle kuwekeza.

b) Utakuwa tayari kufanya uchunguzi wa kina kwenda kuchunguza suala lile ili tupate taarifa ya uhakika kupata kumjua nani muhusika wa tatizo lile. Maana yake suala hili limekuwa la muda mrefu na wananchi walikuwa wakilalamika na lini itaanza safari baada ya matengenezo hayo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri kwa mujibu wa Kanuni jibu maswali mawili (a) na (b). Mhe. Jaku Hashim Ayoub ameuliza karibu maswali manne, utakuwa tayari kufuatana na Wajumbe, Lakini la pili haioni serikali kama kuna tatizo. La tatu akasema kama lini utachukua hatua gani au utachunguza. Kwa hivyo kuna maswali manne Mhe. Jaku Hashim Ayoub umeyauliza. Hivyo Mhe. Waziri nakuomba ujibu maswali mawili kwa mujibu wa Kanuni.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub maswali mawili ya nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

a) Meli sasa hivi ipo kwenye matengenezo. Kwa hivyo siwezi kumchukua mtu yeyote kumpeleka kule kwa sababu ipo katika matengenezo na hatutaweza kwenda na kundi la watu kuingilia utaratibu unaoendelea. Kama mnataka subirini meli ikikamilika tutakwenda hata Baraza zima sina tatizo.(*Makofi*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku naomba utulie Mhe. Waziri ajibu maswali yako.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Suala la pili ambalo ningependa kumjibu ni hilo la kuunda Tume kwenda huko. Sasa kama meli ipo kwenye matengenezo wanakwenda kuchunguza nini, ingekuwa haijakuwa kwenye matengenezo ningekwambieni nendeni lakini meli ipo kwenye matengenezo, watu wanatengeneza wapo kazini, kitakwenda kuchunguzwa kitu gani. Naona kama hilo suala limepitwa na wakati.(*Makofi*)

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu Kifungu cha 37 Mhe. Mwenyekiti, hata mgonjwa akiumwa huwenda akakaguliwa ….

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub sijakuruhu useme. Mhe. Jaku umesema kuhusu utaratibu Kifungu cha 37, ni kuhusu utaratibu Kifungu 63.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kifungu 63 na 37

Mhe. Mwenyekiti: Useme hivyo

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sawa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Kanuni gani imevunjwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: "Waziri au Mjumbe yeyote anayeuliza swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu na kwa sahihi na kwa ufupi ispikokuwa kwamba swali lililoulizwa Waziri mmoja anaweza kujibiwa na Waziri mwengine au Mwanasheria Mkuu", lakini hata hapo kuna nyengine 59 lakini sitaki kuitumia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub sijakuruhusu useme, umesema Kanuni ya 37 kwamba, "Mjumbe yeyote anaweza akasimama ikiwa hajaridhika na jawabu au hajajibiwa kwa usahihi na ufasaha". Lakini Mhe. Waziri ndio amekupa majibu. Kwa hivyo itakuwa wewe una majibu mengine zaidi yake yeye. Hivyo nakuomba utulie tuendelee kubaliana na majibu ya Mhe. Waziri. (*Makofi*)

Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata kwa swali la nyongeza.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Usafirishaji kwa jitihada ambazo zinategemea kwamba serikali yetu inafanya bidii ili kuwaondolea shida wananchi wetu katika usafiri hasa tukitoka Unguja na Pemba, lakini pamoja na hilo kwa kuwa Mheshimiwa kasema wamo katika matengenezo lakini matengenezo yana muda wake. Je! kwa faida ya wananchi wetu wa Zanzibar lini tanategemea meli hiyo itamalizika katika matengenezo hayo ili iweze kutoa huduma zake kati ya Unguja na Pemba na Zanzibar na Bara.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Ali Suleiman Ali meli imeharibika mafundi wamefungua wanatengeneza hawajatwambia lini itakamilika lakini itakapokamilika tutawajulisha.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nikushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimshukuru sana Mhe. Waziri mwenye majibu mazuri *short and clear. L*akini natataka kumuuliza Waziri kwamba katika ripoti yetu ambayo ilisomwa juzi nilisikia kwamba MV. Maendeleo ipo katika jitihada za kutaka kufanyiwa matengenezo ili iendelee na safari zake kama kawaida.

Matengenezo haya kama ni kweli yatafanyiwa katika nchi gani lakini. Je! ni mategemeo maana yake wananchi wengi wamefurahi meli ile kurudiwa, ni mategemeo ya lini meli itaweza kuanza kazi.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Sarahani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kweli meli ya MV Maendeleo itatengenezwa na itakuwa katika jumla ya meli zinazotoa huduma katika visiwa vyetu, huko nyuma kulifanywa *attempt* ya kuuzwa lakini ikawa haikununuliwa kwa bei tuliyoitaka. Kwa hivyo tukafanya maamuzi kwenye Baraza kutokana na hali yake tukaona kwamba hakukuwa na ulazima wa kuitupa meli ile kwa gharama ndogo. Hivyo bora kuitengeneza na kuifanyia kazi kama ilivyo kwa sababu haikuwa mbovu kiasi hicho lakini kwa vile tulikuwa tunajua kwamba tunanunua meli nyengine. Kwa hiyo tukaona kwamba ile basi tuiachie lakini sasa imekubalika kwamba itengenezwe upya, meli ile sasa hivi wanaisafisha ili iweze kupelekwa katika kutengenezwa.

Meli itapelekwa Kenya Chelezoni na katika bajeti ya mwaka huu tulionao pesa ndio zilizotengwa zitatengwa lakini hatujajua ni kiasi gani itakuwa, lakini zimetengwa. Kwa hivyo kwa bajeti hii ya mwaka 2018/2019 matengenezo ya meli hiyo yatafanyika.

Mhe. Mwenyekiti: Ninakushukuru Mhe. Waziri. Katibu kwa shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2018/2019

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea lakini kabla sijamwita mchangiaji ambaye anataka kuchangia siku ya leo, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe.

Waheshimiwa Wajumbe imeonekana kama ndio mtindo sasa hivi wa Waheshimiwa Wajumbe kuhusu utaratibu, ni haki yeni Kikanuni na Kanuni ya 63(1) imewaruhusu mfanye hivyo lakini pia muangalie Kanuni ya 63(2) sio ukisema kuhusu utaratibu ndio tayari wewe uzungumze lakini Kiti kina mamlaka.

Kuhusu utaratibu lakini na kiti pia kikuruhusu, lakini na chengine Waheshimiwa Wajumbe niwakumbushe tena tuzizingatie Kanuni, kwa sababu hili Baraza letu tunaendesha kwa mujibu wa Sheria na kwa mujibu wa Kanuni zetu ambazo tumezifanya sisi wenyewe.

Waheshimiwa Wajumbe baadhi yenu mkisimama baadhi yenu munakuwa hamna imani na Kiti na mtangaza kudhihirishia umma, kwa sababu ukikaa kwenye chombo hichi ukisema chochote tayari umma wote unajua. Mhe. Mjumbe mwengine anaweza akasema nitatumia Kanuni ya 121 kwa sababu tu ya kumuondosha Spika au Naibu Spika au Wenyeviti.

Lakini mkumbuke kwamba hizi Kanuni mnazozitumia nyinyi na sisi ndio tunazozitumia katika kuongoza hili Baraza, isifike pahala tukawa kama tupo katika fete, kama tuko kama tuko sehemu nyengine yoyote. Tutumie Kanuni lakini sio kila mtu ukisimama, mimi sina imani Mhe. Spika naomba Wenyeviti na nani wawe pamoja wafanye hivi, tunaendesha jamani kwa mujibu wa hizi Kanuni ambazo tumezitunga. Sasa wewe kama utakuwa huna imani kwa Kanuni hii hii, kuna Kamati ya Maadili humu, umeona umefanyiwa sivyo basi peleka kwenye maadili na sio kusimama ndani ya Baraza hili Tukufu ukaanza kusema maneno yasioyofaa.(*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe haipendezi hata kidogo kwa sababu sisi tuliokaa hapa mlituchagua nyinyi wenyewe kwa kutuamini. Sasa sidhani kama tutafika pahali tutaendesha vikao vyetu kwa kubishana, twende kwa mujibu wa Kanuni tufuate taratibu, Kiti kinatumia Kanuni hizi hizi lakini nyinyi mnatumia Kanuni hizi hizi. Kwa hivyo yale malalamiko ya kila wakati Wenyeviti, Kiti hamkiamini basi sifikiriki kama tutafika pahala. Sote tunajenga nyumba moja lakini pia niwaambie na mimi natamani sana kwa sababu ni Mwakilishi wa Jimbo na ninatamani sana kuchangia Wizara tofauti tofauti kwa sababu na mimi nina malalamiko mengi basi tuchangie kwa utulivu.(*Makofi*)

Lakini pia tusione kuwa umepata nafasi huko ukawa unazungumza vile vitu ambavyo unahisi wewe vinafaa. Waheshimiwa tusiende hivyo. Mimi nakuombeni sana tuzisome hizi Kanuni, kila mtu mwenye haki yake kwa mujibu ya Kanuni hii ambayo tumeitunga sisi wenyewe basi nina imani haki yake ipo ataipata na tutaifanyia kazi kwa pamoja. Serikali inatumia hii Kanuni kwa sababu wamo humu ndani ya chombo hichi lakini na Wajumbe pia wamo ndani ya chombo hichi tuzitumie hizi Kanuni ipasavyo. Mimi sikurupuki kwa mtoa mtu au kuzungumza kitu chochote kama sijaangalia hizi Kanuni.(*Makofi*)

Kwa hivyo nawaomba sana ukiona hujatendewa haki, tufuate taratibu za Kamati ya Maadili ambayo imo katika hizi Kanuni. Hivyo Waheshimiwa Wajumbe tuzisome na tuzifuate hizi Kanuni nawashukuru sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo katika kuwakumbusha ili twende vizuri katika michango yetu. Sasa mtachangiaji wa mwanzo siku ya leo naomba nimwite Mhe. Nadir Abdul-latif atafuatiwa na Mhe. Omar Seif Abeid na Mhe. Shehe Hamad Matar ajiandae.(*Makofi*)

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba umpatie mwenzangu mimi nitaendelea baadae kwa sababu nilikuwa sijajua na sijawa tayari.

Mhe. Mwenyekiti: Sijakufahamu!

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Sijawa tayari sasa hivi kuchangia naomba umpatie mwenzangu mpaka baadae kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante naomba nimwite Mhe. Omar Seif Abeid. Mhe. Omar Seif Abeid simuoni naomba nimwite Mhe. Suleiman Makame Ali atafuatiwa na Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka fedha 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuchangia kwanza niipongeze sana wizara chini ya Mhe. Waziri *comrade* jembe ambaye kwamba ameaminiwa na Mhe. Rais na ni kweli ni muaminifu, anafanya kazi vizuri, maana yake hata ukitazama kwenye ukusanyaji wa mapato tumefikia asiliamia kubwa ya bajeti ambayo kwamba hii tunayoendelea nayo ya mwaka 2017/2018. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote na hususan zile taasisi za ukusanyaji wa mapato waendeleze jitihada zaidi na waendeleze kasi zaidi, ili kuhakikisha kwamba inakusanya mapato na mapato haya yanakwenda kuwahudumikia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende moja kwa moja kwenye Shirika hili la *PBZ*. Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana *PBZ* nao kwa kueneza *ATM* na huduma zao nzuri wanazozifanya ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma zilizo bora za kifedha na vile vile wao wapo katika mstari mzuri kabisa wa kuhakikisha kwamba hii biashara yao wanaifanya vizuri ili na shirika lile nalo kuweza kupata faida na kujiendesha.

Mhe. Mwenyekiti, niwaomba sana shirika wazidi bidii zaidi kwa sababu Wazanzibari wengi wanategemea *PBZ* ndio kimbilio lao. Vile vile waziboreshe zaidi zile huduma ili wananchi hususani kipindi hiki tunachokwenda nacho cha siku kuu na vipindi vyengine wasipate kusumbuka waende vizuri, ili wazidi kuifurahia Benki yao ya *PBZ*.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye suala zima la viinua mgongo kwa wafanyakazi wastaafu. Mhe. Mwenyekiti, kuna Mhe. Mjumbe mmoja hapa alizungumzia suala hili na mimi naomba nilisemee kidogo. Mhe. Mwenyekiti, suala hili naiomba sana serikali kwa kupitia wizara kuhakikisha kwamba wale wafanyakazi ambao wameshalitumikia taifa hili, basi inapofikia muda wa kustaafu kile kiinua mgongo chao wapewa kwa wakati ili waweze kufanya yale walioyakusudia wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kama unavyojua kuna wengine huwa wanataka kwenda kukamilisha ile nguzo ya tano ya Kiislamu ya kwenda Makka kuhiji na pia wengine wana mipango yao mbali mbali ya kufanya, lakini wanapochelewa kupata pesa hii basi inafika mpaka yale mambo mengine yale waliyojipangia kuzorota. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri nina imani kwamba analifanya hilo na sio jambo gumu la hivyo, lakini namuomba sana Mhe. Waziri awafikirie zaidi kwamba mtu anapostaafu, basi na ile kiinua mgongo chake asikae miaka mingi, mwaka mmoja

hadi miwili aweze kupewa kwa muda wa miezi kama mitatu. Kwa sababu mipango ipangwe mapema ili ijulikane kwamba *list* hii wakifika mwaka huu wanastaafu na ikifika wakati wao wa kustaafu basi na kiinua mgongo chao kuweze kuwafuatia, ili kuondokana na ule usumbufu wa kufuata mawizarani kwenda kudai viinua mgongo. Ni jambo zuri sana hilo na pia litawajengea imani wananchi wetu ili kuhakikisha kwamba pale walipolitumikia taifa hili itakuwa hawajuti. Nina imani Mhe. Waziri hilo atalitekeleza.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye kuna mradi mmoja nadhani sijui ni *ZUSP* sijui ni nini uko chini ya Wizara ya Fedha mradi ule. Mhe. Mwenyekiti, nitazungumzia Pemba. Sasa hivi pale Chake Chake ni mji mkubwa sana, ndio mji wetu mkubwa tunaouringia kwa Pemba lakini Mhe. Mwenyekiti, mji ule kuanzia *airport* mpaka Machomanne, mpaka Tibirinzi kwa Bi. Ashura kule ukifika usiku ni kiza totoro, hakuna taa zile za barabarani. Hivyo namuomba Mhe. Waziri alifikirie hili nalo, kama ingekuwa sio zile simu zilizoingia siku hizi za kupangusa ikawa kila mtu anakwenda na kuchati mwenyewe anakwenda akiangalia simu basi ningekuambia wengine ingekuwa tunagongana usiku ni kiza. Ninamuomba sana Mhe. Waziri ule mradi uweze kuharakishwa zaidi ili uweze kufika nako kule Pemba, kuanzia Machomanne *Airport* kule mpaka kufikia Tibirinzi kwa Bi. Ashura.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimkumbushe tena Mhe. Waziri na kila siku nazungumzia suala hili la *ATM*. Mhe. Mwenyekiti, katika jimbo langu Mhe. Waziri nadhani hili hatolipinga na nina imani atalikubali, kwa sababu Wesha anakujua ni vizuri zaidi wale wananchi wangu wa Wesha wakaweza kuwekewa *ATM* ili wapate huduma hii na kuondokana na usumbufu wa kufuata masafa marefu ya kwenda mjini na kwa sababu kutokanana kule Wesha sasa hivi kuna bandari na kumekua vizuri na pia wale wananchi wangu wa Birikau, Tondooni, Kijangwani na Ndagoni wataweza kwenda kutumia huduma hiyo. Namuomba sana Mhe. Waziri alifikirie sana hili kwa moyo wa imani kabisa kwa sababu kuna siku hata yeye anaweza kwenda pale hoteli ya Wesha akapumzika pale akaishiwa pesa, lakini *ATM* ipo anakwenda kuvuta tu. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri hili alifanyie kazi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye huu mradi wa kupunguza umaskini. Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana serikali kwa kuhakikisha kwamba wananchi walio wengi wanapata kwenye masuala mafao haya. Hata ukienda kwenye *TASAF* utayakutia masuala ya upunguzaji umaskini ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanajikwamua na hali ya kiuchumi. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri na hili alifikirie zaidi kama alivyoliweka kwenye kitabu ili tuhakikishe kwamba pesa hii iliyoombwa au iliyokusudiwa kupatikana basi ipatikane ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanaondokana na ukali wa maisha.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye Mfuko wa Barabara. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri juzi alisema hapa kwamba hadi kufikia hivi sasa Mfuko wa Barabara umetumia asilimia 26. Kwa hivyo mimi namuomba sana Mhe. Waziri ahakikishe kwamba ile pesa inapotengwa itumike kama ilivyokusudiwa, lakini vile vile ziangaliwe barabara za ndani zaidi nazo ili kufanyiwa marekebisho ikiwemo na ile barabara yangu ya Ndagoni pamoja na kule Michungwa jimboni kwangu katika Jimbo la Ziwani.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye miradi ya wizara. Mhe. Mwenyekiti, niipongeze tena hapa wizara kwa kuona kwamba ile miradi waliyojipangia kama yale majengo ya serikali yanayojengwa pale Gombani, kuhakikisha kwamba serikali inatokana na kodi ili kupata majengo yake na kuweza kuyatumia majengo yale bila ya usumbufu wowote na kuondokana na ile kodi ambayo kwamba pesa ile ilikuwa iende kwenye sehemu nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo zuri sana naipongeza serikali kwa kupitia Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein ambaye wazo hili nina imani alilileta yeye, lakini pia msimamizi wake Waziri wa Fedha na Mipango akaweza kulisimamia vizuri ipasavyo.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi ya kuchangia isipokuwa namuomba Mhe. Waziri na wala sitompiga buti, kwa sababu najua kwamba ni mtendaji, ni mwaminifu, ni msema kweli na ni mchapakazi. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri haya niliyomshauri ayafanyie kazi ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata maendeleo kila kukicha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia, haijawahi kutokezea kuchangia bajeti yoyote kwamba nisizuwia kifungu. Lakini bajeti hii Mhe. Waziri kwa ninavyomjua nina imani ataweza kuyakamilisha.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Suleiman Makame kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Shehe Hamad Mattar, simuoni Mhe. Machano Othman Said. Naomba nimwite Mhe. Jaku Hashim Ayoub na atafuatiwa na Mhe. Ahmada Yahya.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru na nianze kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake na wafuatiliaji wake, sina mashaka naye Mhe. Waziri na nimuombe tu afya njema na umri mrefu, ili nia yetu ile ya mbele kama Mwenyezi Mungu akitujaalia salama iwe vizuri, safari yetu ya matumaini.

Mhe. Mwenyekiti, nitaanza na kadhia ya *FBME Bank.* Kwa masikitiko makubwa sana na kwa unyonge na kwa huruma sana na benki hii imewagusa wengi na wengine tumo ndani humu, mmoja na mimi nikiwemo na mstari wa mbele huko wamo naamini wameguswa. Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana kuna watu wanadaiwa wanataka kupelekwa Mahakamani pesa zao ziko pale wananyanyasika, wengine wameshaanza kutangulia mbele ya haki kwa Mwenyezi Mungu, ni usumbufu mkubwa mno. Suala hili nimeshalifanyia kazi Dodoma lakini na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mkono wake kama serikali na hii benki ipo Zanzibar, nafikiri ndio Makao Makuu yake, malipo yanakuja Zanzibar, usajili Mhe. Mwanasheria Mkuu nisaidie umefanywa Zanzibar upo, *Certificate of Compliance* imetoka Zanzibar, leseni ya biashara imetoka Zanzibar. Mhe. Mwanasheria Mkuu vitu hivyo, sheria ya Zanzibar zinatumika katika benki ile. *Only* kitu kimoja tu *regulator* ni Benki Kuu.

Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani serikali isiwe na majibu ya suala hili, narudia tena kwa mara ya tatu, haiwezekani serikali isiwe na majibu ya suala hili. Mhe. Mwenyekiti, wanalipa *ZSSF*, *ZRB* na *TRA*, kwa hivyo Zanzibar tuna mkono wetu lazima tufike pahali wananchi wanateseka,

wengine wanataka kuwasomesha watoto wao wanakosa elimu, wengine wanataka kufanya biashara ndogo ndogo wanakosa na kuna wawekezaji wanaumia nao. Kubwa tunaambiwa zile pesa ziko salama, usalama wenyewe upo wapi miaka mitatu au minne. *Greenland Bank* ilifungwa haikuchukua muda. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo Mhe. Waziri atakapokuja atupe jawabu, msingi niliyoutaja usajili umefanywa Zanzibar, *Certificate* ya Zanzibar, leseni ya biashara ya Zanzibar na benki inatumia ni sheria za Zanzibar, watu wanateseka miaka mitatu au minne na dhamana ni Benki Kuu, muda mrefu. Mimi najua kuna Waheshimiwa Wajumbe watakuwa wanalifurahia sana suala hili leo.

Kwa hivyo kaa kitako na Mhe. Waziri wa Fedha Dkt. Philip Mpango na nilishamwambia Dkt. Philip Mpango akasema serikali imelichukua na italifanyia kazi. Kama Kanuni zinavyoelekeza hapa, nilisimama baada ya maswali na majibu Bungeni nikaiomba serikali. Tukaambiwa tumelichukua suala linafanyiwa kazi lakini mpaka muda huu nipo hapa sijafika Dodoma kwenda kulifuatilia suala hili. Lakini hairidhishi wawekezaji na pesa zao wanataka kuwekeza kwa muda mrefu wamekwama. Kwa suala hili Mhe. Waziri mtafute Dkt. Philip Mpango, nyinyi ndio wenye dhamana na muna dhamana kwa wananchi na hata wananchi wa Donge naamini watakuwa wana pesa zao kule, ninavyoamini kwa hii cheo ni dhamana na itabidi siku kuu hii watahitaji matumizi watu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala la *ZMA*. *ZMA* ilikuwa ikipokea ruzuku kutoka serikalini, ilifika wakati *ZMA* ikawa inachangia Mfuko Mkuu wa Serikali yaani Hazina karibu milioni 40 kwa mwezi kwa harufu niliyoipata. Sasa hapa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri je, suala lililokuwepo wanachangia tena kiuchumi katika mfuko huu *ZMA* na kuna ofisi zao kule Dubai zimefungwa.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika 4.5 ya mgao wetu. Mhe. Mwenyekiti, hii *formula* ni ya zamani na ya muda mrefu na Zanzibar imekuwa na hata *population* yake imekua 4.5 ya mgao. Ninavyokumbuka mimi tokea nafumbua jicho mpaka hapa nilipofika ndio hii 4.5 ya mgao wetu kutoka Tanzania Bara ni ya muda mrefu, ni lazima ifike pahala itafutwe *formula* Zanzibar imekua, *population* imekuwa, mji umekuwa, barabara zimeongezeka na magari yameongezeka, kwa suala hili nitahitaji maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini isitoshe kuna mashirika ya Muungano kama *NMB*, Posta, *TCRA* Mhe. Waziri ukija unielimisha kidogo ndio kama nilivyokueleza elimu yangu mimi ni ndogo tumepata nini, *ATCL* tumepata nini Zanzibar katika mambo haya ya Muungano. Ninachokijua tu hata *NMB Bank* ni shirika la Muungano vile vile, tumefaidika vipi katika mambo kama haya. Kuna Bima nayo nimesahau uje unieleze kidogo. Ninachojua mimi nafikiri Benki Kuu (*BOT)* ndio tunaopata mgao kwa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna *issue* kidogo nayo ya *VAT*. Mhe. Mwenyekiti, mwaka 2016, 2017, 2018 na 2019, *ZECO* inanunua umeme kutoka Tanzania Bara kwa *bulk*. Sasa kinachoonekana kule Bara, hata hawa *Twiga Cement* au *Tanga Cement* bei wanayouziwa wao na sisi tofauti, ni sawa sawa sio tofauti nifute kauli. Bei wanayouziwa *Tanga Cement*, *Twiga Cement* na sisi Zanzibar tunaonunua kule ni bei moja. Hapo zamani ilikuwa kuna *formula* kidogo ilikuwa chini kwenye malipo. Kwa hivyo hapa Mhe. Waziri aje anieleze kidogo hii *bulk* tunayonunua

makubaliano ya zamani iwe rahisi ndio makubaliano yetu kununua umeme kutoka *TANESCO*. Mhe. Mwenyekiti, umeme huu tunanunua kutoka Tanzania Bara lakini cha kushangaza na cha kusikitisha miundombinu ni yetu tuliyotandika *submarine* zile *cable* tulizotandika baharini ni zetu. Haiwezekani umeme ule sisi tukanunuwe kule kwa bei moja na viwanda. Kwa hili kidogo Mhe. Waziri uje unieleze *submarine* zetu, *cable* zetu na hili *ZECO* ni shirika la serikali lazima tuwasaidie.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye *TRA* tuko vizuri nashukuru sana, lakini kidogo tu hapa kwenye mambo ya ajira ni mambo ya Muungano kidogo lifanyiwe kazi. Mhe. Mwenyekiti, halafu nije kwenye *ZRB*. Niwapongeze *ZRB* kwanza wanafanyakazi vizuri lakini mengine yanataka tutumie akili na maarifa. Haiwezekani gari imekaa kwenye *parking* unakwenda kufungua *plate number* unasema hii ni *taxi,* ushahidi mnao. *ZRB* mko juu, ushahidi mnao kuwa hii ni *taxi,* gari ime-*park* tu munakwenda kuifungua namba. Sio kitu kizuri na sio kitu cha kiungwana kwa desturi zetu na mila zetu za Kizanzibari. Kwa jambo hili *ZRB* tusijaribu kutumia nguvu, kodi haikusanywi kwa mtutu wa bunduki wala nguvu, hekma na busara ni kitu muhimu, mujitahidi kazi nzuri, ni kukumbushana tu. Mhe. Mwenyekiti, unajua timu ya mpira kocha ndio anayeiona zaidi kuliko wale wachezaji waliokuwepo juu. Kwa hili kidogo twende na kauli kidogo zilizokuwa nzuri hasa mwezi huu Mtukufu wetu huu wa Ramadhani.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kuna kilio cha fedha watu wanakwenda kununua mizigo Dubai wamekuwa wakipata usumbufu uwanja wa ndege. Huku tunataka biashara na huku tunasema nguruwe haramu lakini mchuzi wake tunaunywa. Mhe. Mwenyekiti, watu wanasumbuka na pesa zao 20,000 au 30,000 na huwezi kutuma *TT bank.* Hili liangalie kuna watu pesa zao zimekaa muda mrefu, zimechukuliwa hakuna kinachoendelea na sio kuwa wanapewa faida. Mhe. Mwenyekiti, hili suala kaa ulifikirie ili biashara iende na hii ni fedha kwa mambo haya yatahitaji maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*). Nimpongeze sana Mkurugenzi wa benki ile. Nimuombe tu sana ajaribu kuliangalia suala la *ATM* halijakaa sawa mpaka hivi sasa pamoja na jitihada au kelele tunazopiga humu ndani au mchango wetu humu ndani, lakini bado *ATM* zimekuwa zina usumbufu. Mhe. Mwenyekiti, tulipotoka na tulipofika ni tofauti, maendeleo tumeyaona lakini bado usumbufu na foleni kuwa kubwa hasa Tawi la Mwanakwerekwe. Hili Mhe. Mwenyekiti, liangaliwe.

Mhe. Mwenyekiti, suala la *parking* ya benki ya Mperani imekuwa wananchi wanapata usumbufu katika *parking*. Mhe. Mwenyekiti, unafuata huduma pale, benki inalipa kodi zote na wewe mwananchi ukienda kule Manispaa wanakusubiri wakutandike. Kwa suala hili nalo ufike pahali uliangalie.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nafikiri nimuombe tu Mhe. Waziri kidogo baadae huko mbele tukishapitisha bajeti yetu haraka sana aiangalie Wizara ya Afya kuwapa pesa kwa haraka ili tukafanye kazi za wananchi. Mhe. Mwenyekiti, kuna mengine nafikiri nitapeleka mchango wangu kwa maandishi.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nitahitaji maelezo zaidi na nitazuwia kifungu katika mambo ya benki, naomba liandikwe hilo nisije nikafika pahali nikajakuambiwa mimi sijaandika masuala ya benki hapa nitahitaji maelezo.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil, atafuatiwa na Mhe. Waziri asiye na Wizara Maalum Mhe. Said Soud .

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi asubuhi hii kushiriki katika uchangiaji wa bajeti hii ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuishukuru Wizara hii ya Fedha na Mipango na watendaji wake wote, kuanzia Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, na Makamishna wote kwa jinsi wanavyosimamia utendaji mzuri katika wizara hii.

Kwa heshima zote na kwa taadhima naomba sana Waheshimiwa Wajumbe wakati wa kupitisha bajeti hii, sote tuungane kwa nia moja ya kupitisha bajeti hii ambayo ni bajeti mkombozi kwa nchi yetu. Hakuna asiyeelewa kwamba hotuba hii imeonesha vipaumbele vyote, sio vipaumbele tu lakini viashiria vyote, kila swali lina jawabu lake, ziko changamoto mbali mbali. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kila changamoto ina jawabu lake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu bajeti hii tuipitishe kwa asilimia mia moja, kusiwe na buti ya aina yoyote. Ushauri wangu mdogo tu uko kwenye Tume ya Mipango, kwamba tume inafanyakazi nzuri sana mashirika yake, wakati umefika kwamba Tume ya Mipango iwe na Kitengo cha *Technical Committee*. Kitengo hiki kinahitajika muhimu sana ili kiweze kuchanganua miradi mbali mbali, thamani ya mradi na fedha zitakazoidhinishwa katika mradi ule. Mhe. Mwenyekiti, katika semina waliyotufanyia Kariakoo tulizungumza suala hilo na leo hapa Barazani kwa heshima kubwa naomba suala suala lile tuzungumze na iundwe *Technical Committee* ili iweze kuchambua na kuchanganua thamani ya miradi mbali mbali.

Baada ya kusema hayo mimi Mhe. Mwenyekiti, sio mtu wa dakika nyingi. Kwa heshima na taadhima na kwa wenzangu wote Wajumbe wa Baraza hili tukufu, nawaomba tumpigie kura asilimia mia moja bajeti hii na mimi natamka rasmi kwamba naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja na zaidi.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Ahmada Yahya kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum Mhe. Said Soud Said.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi nikazungumza kuhusiana na suala zima la mchango wa bajeti hii

ya Wizara ya Fedha na Mipango ambayo kwa kiasi kikubwa imeelekeza mambo mengi sana katika nchi yetu na hususan yale ambayo yanategemewa kufanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mazingira ya kuwaletea watu maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nisome ukurasa wa 42, "utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2017/2018 kwa taasisi zinazosimamiwa na Wizara na Bodi ya Mapato ya *ZRB"*. Mhe. Mwenyekiti, mahesabu haya na mengine yote yaliomo humu ni sawa sawa na lengo kubwa ni kuelimisha Wazanzibari juu ya utendaji mzuri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hivyo nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutokana na uongozi wake mahiri wa kujali shughuli mbali mbali zinazohitaji fedha katika nchi yetu na akawa tayari fedha hizo kutumika ili wananchi waweze kufanikiwa.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nachukuwa nafasi kumpongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wake kutokana na jitihada kubwa wanayoichukuwa katika kuendeleza na kudumisha utawala bora, maana utawala bora ni pamoja na fedha. Sasa mazingira ya fedha katika nchi yetu alhamdulillahi yanafika pahala kwamba tumshukuru Mwenyezi Mungu kutokana na uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein, usimamizi wa Wizara hii kupitia |Waziri mwenyewe ni jambo la kufurahisha sana.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jambo la pili ambalo nilikuwa nataka nizungumze ingawa uliligusa, lakini na mimi sina budi niliseme na niliseme kwamba nilianza tokea jana kusema na Wajumbe mbali mbali. Natumia Kanuni ya 45 kifungu cha 1 Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana juu ya suala zima la baadhi ya Wajumbe kutumia Kanuni hii vibaya. Kanuni hii inatumika vibaya.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri Soud Said Soud suala la Kanuni kwa kweli nimelitolea ufafanuzi, nilikuwa nakuomba uende zaidi kwenye mchango wa Wizara, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa. *(Makofi).*

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana lakini nilikuwa nataka niseme tu kwamba kwa sababu kifungu hiki kimempa nafasi Mjumbe kwa kibali cha Spika labda kwa sababu hutaki kunipa kibali cha kusema basi nitanyamaza na mchango wangu utaishia hapa.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Soud Said Soud ukisema sijakupa kibali cha kusema utakuwa hujakitendea haki Kiti. Nimekupa nafasi ya kusema na hapa uliponiletea maombi umetaka kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na ndio maana nikakwambia suala la Kanuni tayari nimeshawafahamisha Wajumbe. Kwa hivyo ile tayari nimeshawapa na nimeshawaambia, wewe ulikuwa ujikite kwenye Hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango lakini kama umeridhika na umeishia hapo, basi na mimi nakushukuru.

Sasa naomba nimwite Mhe. Panya Ali Abdalla atafuatiwa na Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote sina budi na mimi nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataallah ambaye ametuamsha tukiwa hatujambo wazima wa afya, lakini na wale ambao amewahitaji, basi Mwenyezi Mungu awape safari njema na awajaalie malazi mema, lakini na sisi atupe mwisho mwema na atulipe fadhila kubwa ambazo amezipanga katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaendelea kwanza nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, nampongeza nanichukuwe fursa hii kuwashukuru wale Wawakilishi wenzangu wote waliompongeza na kumtakia heri juu ya kazi zake Mhe. Waziri huyu wa Fedha na Mipango. Naungana nao kwa asilimia mia moja na kwa sababu kila walivyokuwa wakitoa pongezi zile ilikuwa mimi wananizidishia afya kubwa, kwa sababu mimi ndiye Mwakilishi wa Jimbo langu la Donge. Kwa hivyo wale wote ambao wamempongeza walikuwa wakitupongeza wananchi wa Jimbo la Donge kwa uamuzi mkubwa na mzuri ambao tumeweza kumchagua mtu makini ambaye anastahiki sifa hizo na kuongoza Baraza hili na anastahiki kuongoza pahala popote ambapo anaweza kupangiwa na serikali hii. *(Makofi)*

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi nichukue fursa hii kumpongeza sana lakini pongezi hizi hazitakuwa sahihi kama sikumpongeza Rais wangu wa Zanzibar ambaye nidye aliyemteuwa Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed. Kwa hivyo namshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kututeulia kijana huyu ambaye ni kijana mchapakazi, mwenye ujuzi kabisa wa kazi yake lakini ni msikivu na ni mfanyakazi kwa mashirikiano na wenzake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka niyaseme hayo lakini mimi mchango wangu katika hotuba hii nilitaka kwenda katika suala zima la kusimamia upatikanaji na utowaji wa takwimu. Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Waziri na hasa pale walipotuonesha kwamba sasa watashughulika sana na mambo ya takwimu. Hatua ya mwanzo ni kutuonesha jengo lile ambalo wamelijenga na ni la kisasa zuri na litaweza kweli sasa kufanyika kazi hiyo. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana suala zima la mipango yote ya serikali kama itakuwa haina takwimu zilizo sahihi, basi tunaweza tukajikita hapa kufanya mambo chungu nzima lakini yakenda *wrong* kwa kukosekana takwimu zilizo sahihi. Kwa hivyo naomba nichukue fursa hii kuomba sana, kwa sababu hapa wizara zilizopita kulikuwa kuna masuala ya udhalilishaji kila wizara tunapata takwimu yake, iliyokuwa sahihi ni ipi. Kwa hivyo mimi naomba sana hili suala la takwimu ndio linaweza kutuweka sisi katika mipango yetu mizuri ya serikali na utekelezaji wake ukaweza kwenda vizuri kutokana na suala zima la takwimu.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo hiki kisimamiwe vizuri na naamini tunaweza tukafikia pahala pazuri. Lakini suala la takwimu nataka kulisema hasa pale inapofanyakazi sasa ya sensa ya wananchi wa nchi hii. Mhe. Mwenyekiti, kuna watu huwa wanapinga tu suala hili la kutokwenda kujiandikisha ili takwimu hizi zikaweza kupatikana katika usahihi wake. Mhe. Mwenyekiti, naomba suala hili litakapojitokeza likemewe na sheria ichukuwe mkondo wake, kwa sababu inarejesha nyuma mpango mzima wa serikali ambao unakusudia mimi nimepata kitu hiki nikigawe vipi kwa wananchi wangu, unashindwa unapotaka kukigawa unakuja kukuta watu walaji wapo wengi, lakini wakati wa kujiandikisha walijitokeza wachache. Kwa hivyo naomba sana kitengo hiki kiweze kufanyiwa kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia nikienda katika ukurasa wa 58 kuma mradi wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge (MKURABITA) huo. Mhe. Mwenyekiti, niombe sana mradi huu ni kweli tuna watu wanyonge na tunasema tunapambana nao ili tuweze kuwatoa katika unyonge ule, kuwatoa katika umaskini angalau na wao waweze kuwa watu wa kawaida. Mhe. Mwenyekiti, wanyonge hawa tuwaangalie sana katika masuala haya ya ardhi. Serikali lazima ione pale inapokuwa ina maeneo basi iweze kuyapima na wale wanyonge tuweze kuwapatia ili waweze kumiliki ardhi. Kwa sababu mnyonge wa Mwenyezi Mungu anakwenda kujenga mahala ambapo hapastahiki, matokeo dhoruba zile zinapompata pia serikali inagharimika kwa mtu yule, lakini pia yeye kama pengine amejenga pahala sipo atakumbwa na kadhia ya kubomolewa nyumba yake ile tutakuwa hatukumpunguzia umaskini ila tumemzidishia umaskini. Kwa hivyo mimi naomba sana kuwaangalia wanyonge hawa na kuwainua katika vipawa vyao hivi vya biashara ili hatimae na wao waweze kujitegemea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mambo mengi ya kuzungumza katika Wizara hii kwa sababu hii ni ndio Wizara mama ambayo tunategemea, Wizara hizi zote tulizokuwa tukiziombea hoja zake hapa, tulizokuwa tukiziombea fedha hapa bila ya kumruhusu Dkt. Khalid kuchakarika sana akaweza kutuletea mapato tukaweza kufanya matumizi inaweza tukafanya kazi ya zeze. Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri tangu alivyoingia madarakani kushika Wizara hii tumeweza kuona mabadiliko siku hadi siku ya ongezeko la mapato. Hivyo tunamtakia heri na tunamuombea bado aenda akasimamie vyanzo vyetu vya mapato hivi bado mivujo ipo. Kwa hivyo tunaamini tunaweza kukusanya zaidi ya hizi ambazo tunazo.(*Makofi*)

Kwa hivyo tunakutakia heri na mimi niombe tu kwa Waheshimiwa wenzangu huyu mwenzetu ni mbuninifu, mchakarikaji ni mtafutaji, tumuachie aende akazitafute fedha ili Wizara zetu ziweze kufanya utekelezaji wa kazi zake kama zilivyopangiwa. Ninaamini chini ya uongozi wake tunaweza hata tukimaliza miaka mitano hii Wizara hii atakuwa ameifikisha mahala pazuri sana. Mimi nikuombeni tu wenzangu tusipige mabuti pale, tumpe moyo wa kwamba kazi aliyoifanya inaonekana na sisi inaturidhisha na tunamuomba aendelee kuifanya ili Serikali hii iweze kupunguza utegemezi.

Mhe. Mwenyekiti mimi nichukue fursa hii tena kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, niseme kuna siri ambayo nimeigundua ya Mhe. Rais kufikia mafanikio haya na naomba niiseme siri hiyo Mwenyekiti wa UWAWAZA kama upo naomba unisikilize au wale wanawake wenzangu popote walipo naomba wanisikilize. Mhe. Mwenyekiti, siri moja ya Dkt. Shein kuweza kuyafikia mafanikio haya kwa kina si jengine ni kuwa na Mheshimiwa Mama yetu Mwanamwema Shein ambaye ameweza kutuliza fikra na akili za Mhe. Rais wetu, amemlea baba yetu huyu kwa busara kubwa. Kwa hivyo ameweza sasa kuyafikia yale majukumu yake vizuri kwa sababu ana utulivu, akirudi hata akipata makero kazini, lakini mama wa kumtuliza nyumbani yupo na anaweza kufanya kazi hizi bila ya hofu. Hongera sana Mama Mwanamwema Shein na nimuombe Mwenyekiti wa UWAWAZA tufanye siku tukamtembelee mama huyu kwa kumpa pongezi za dhati, kwamba amefanya kazi nzuri na anaendelea kuifanya na tunamuomba aendelee kuifanya ili Rais wetu aweze kutufanyia mambo mema na mengi mazuri.(*Makofi*)

Lakini pia pongezi hizi nazitoa kwa Makamu wa Pili wa Rais pia mama yetu ameweza kufanya kazi nzuri ameweza kushirikiana na sisi vizuri, kwa hivyo tumepata uvulivu, tumepata viongozi ambao wanatutuliza, pia kwa Dkt. Khalid pia ama yetu tunampongeza na tunamuomba azidi kuwa mtulivu kwa sababu baba yetu yule ana kazi kubwa ya kutafuta mapato ya nchi hii na sisi tuweze kutumia mapato hayo.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nachukua fursa hii kuiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja na nawaomba wenzangu wote waiunge mkono bajeti hii kwa asilimia mia, kwa sababu mwenzetu ni mchakarikaji ni mtafutaji na Inshaallah Mwenyezi Mungu atatufikisha salama kule tunakotaka kwenda ahsante sana.(Makofi)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Bipanya kwa mchango wako nadhani Mwenyekiti wa UWAWAZA amekusikia na atafanyia kazi ombi lako. Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamuita mchangiaji Mhe. Mohammed Said Mohammed naomba nitoe taarifa kuhusu wageni wetu wa leo. Wageni hawa ni wanafunzi kutoka Skuli ya *FEZA SECONDARY* iliyopo Zanzibar. Jumla yao ni kumi na nne ambao wanaongozwa na walimu wao wawili.

Mwalimu wa kwanza ni Mr. Suleiman Nahoda na wa pili Mr. Khamis Haji. Vile vile wamefuatana na viongozi wao wa Serikali ya Wanafunzi ambaye ni Ndg. Manal Ahmed, Ndg. Ahmadin Islam na Ndg. Abubakar Amour karibuni sana.(*Makofi*)

Tangazo jengine wajumbe wa *CPA* na *CWP* wanakumbushwa kikao muda huu wa saa nne.

Tunaendelea Mhe. Mohammed Said Mohammed.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kwa kushukuru sana na mimi leo nitakuwa sina mchango mkubwa sana, lakini nimesema madamu mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na bajeti hii ndio ipo kwangu, nasema basi angalau nikohowe ili basi kuweza kuiweka hii bajeti sawa. Lakini nipingane sana na Mhe. Yahya Abdulwakil yeye aliyesema bajeti hii ipite itakuwa sio bajeti, tutakuwa tunaanza stori tu, lakini sasa bajeti hii ipite lakini tukiona basi na changamoto zake tulizokuwa tumeziona mara iliyopita tuweze kuziondoa ili Mhe. Waziri akatekeleze majukumu yake ipasavyo.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpa pongezi nyingi sana Dkt. Khalid Salum Mohammed kwa uwasilishaji wake mzuri sana wa hotuba hii, lakini vile vile nimpe pongezi nyingi ndugu yangu Khamis Mussa Omar kwa kazi kubwa anayofanya. Lakini nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitompa pongezi nyingi sana Kamishna wa Bajeti Mwalimu Mwita, lakini vile vile na wasaidizie wao na Kurugenzi zote zilizokuwa zimeambatana nazo.

Mhe. Mwenyekiti, nataka *declare* kwanza kabla sijaanza kuchangia mimi si mchumi, fani yangu ni *medical*. Sasa nataka niseme hili kwa sababu kuna vitu nitavisema na nimeviona naona havinipi afya kama nitaweza kuvisema.

Kwanza tu nataka kwenda kwenye program ya mfuko mkuu wa Serikali. Katiba ya Zanzibar imetuelekeza kwenye kifungu cha 35, lakini vile vile program hii imetuelekeza kwenye kifungu cha 110 na kifungu vyengine jinsi ya mfuko huu wa Serikali unavyotaka kutumiwa.

Mhe. Mwenyekiti, tukija kwenye kitabu kikubwa tunaangalia mambo yote ambayo yamo lakini moja tumesema matumizi mbali mbali. Sasa unaponiambia matumizi mbali mbali nilikuwa tu nataka kujua kwa urahisi sana matumizi mbali mbali yepi. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakapokuja aje anieleze hayo matumizi mbali mbali kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ni matumizi yepi. Maana tumewekea pesa nyingi sana pale hofu yangu lisije likawa chaka tukaweza kuzitumia fedha za wananchi vibaya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee mbele na hili Mhe. Waziri aweze kunijibu na kama hili hatoweza kunijibu vizuri ningeomba nionyeshe nia ya kuweza kushikilia Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye program ya mipango na nili-*declare* kuwa mimi siyo mwanauchumi lakini Mhe. Mwenyekiti, kwanza nisome tu moja katika hizi. Nataka kuanza kuisoma kwa ruhusa yako naomba ninukuu "Programu hii ina lengo la kusimamia shughuli za utendaji na utumishi ndani ya Tume ya Mipango na kuhakikisha kazi zote zinatekelezwa kwa umakini na ufanisi, programu hii ina programu ndogo moja iliyotengewa jumla ya shilingi 1.7 bilioni hadi kufikia mwezi wa Machi 2018 programu hii imetumia jumla ya shilingi milioni 821 sawa na asilimia 48 ya makadirio ya kutekeleza shughuli zake".

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Katibu Mtendaji pamoja na watu wake, lakini nataka kusema asilimia 48 hadi kufikia mwezi wa Machi na ndiyo huu nimesema mimi si mchumi nitakalolikosea ndiyo mlichukulie tu na mradi huu wa kupanga mipango ndiyo mzizi wa serikali yetu lakini ndiyo mzizi wa taifa letu. Sasa ikiwa leo imepata asilimia 48 utekelezaji huu unakuwaje. Lakini vile vile kuna miradi mingapi nataka kujua miradi mingi kwa sababu huu ndiyo mzizi miradi mingi katika wizara mbali mbali ambao Tume ya Mipango ndiyo inayoshauri hata ukipelekea miradi mikubwa yeye ndiye anapaswa kuishauri serikali katika wizara mbali mbali ambazo zipo. Mhe. Mwenyekiti, sipati afya sana na Tume ya Mipango inapanga mipango gani kuna wachumi pale wengi wamebobea lakini mipango gani ya serikali hebu tuambiwe.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwenye kitu kimoja tu kidogo kuna sheria ya *PPP*. Hhebu Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri uniambie Sheria hii ya *PPP* tangu imeundwa tunaona ni makampuni au miradi gani inavyoendelea ipi, lakini sheria hii mimi nimeona ina mapungufu mengi kwa sababu haiwezekani kuwa taasisi moja au kampuni moja inakwenda kuibua miradi halafu mradi ule ule utangazwe tenda na yeye mwenyewe akiwa ana *bid* wakati ameshatumia kazi kubwa sana ya kuweza kufanya vile vitu na kwa ubunifu mkubwa. Kwa hivyo nataka Mhe. Mwenyekiti, niambiwe Sheria hii Mhe. Waziri yeye kama ameiona *advantage* yake nini na *disadvantage* yake nini lakini vipi kama tutaifanyia marekebisho ushauri wangu ni kuifanyia marekebisho kwa ushauri wangu ni kuifanyia marekebisho ili tuone basi *PPP* inakwenda kwa urahisi siyo kujibanabana kama ilivyokuwa.

Lakini miradi mingi mingi inakwama kutokana na sheria hii mimi nasema ni sheria kandamizi na sipo sana rafiki na sheria hii. Ningeomba Mhe. Waziri au serikali ijitahidi kuipitia ifanye mapitio ya sheria hii lakini kama inawezekana ailete Barazani kwa kuibadilisha na kuiweka sawa ili tuweze kuitia nyama na tuweze kuona hali nzuri inaweza kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, labda niende kwenye *ZIPA.* Niwapongeze sana Mkurugenzi Mtendaji wa *ZIPA* lakini na Kurugenzi zake zote kwa kazi kubwa sana anazozifanya. Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa tumetembea nao katika *EPZ* ya *economic zone* ile ya Dar es Salaam na kuona jinsi gani wanavyofanyakazi wenzetu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, atakapo kuja Mhe. Waziri anambie ni jinsi gani wanaweza kuitumia ile *economic zone* yetu ya Amani baada ya kukaa majengo makubwa, majengo mabovu hayana maana kwa sasa yale ni *resources* tunazitumia vibaya. Aje Mhe. Wizara anambie mipango yake ya baadae ni mipango gani ya kuweza kuzitumia *economic zone* kama ile.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana kamati yangu ilipiga kelele ya kuongezewa pesa *ZIPA* za kuweza kujenga uzio mkubwa wa pale Amani. Mwaka huu sijaona kwenye programu hii akija Mhe. Waziri anambie kuna nini kwa sababu mali za watu wengi ma-*investors* wengi zimo mle na ukuta ule umepitwa na wakati ni mfupi mno. Sasa lazima kujengwe ukuta uliokuwa mzuri lakini vile vile na mali za watendaji pale ziweze kusitirika.

Mhe. Mwenyekiti, niliwahi kutoa hoja yangu ilikuwa ikisema taasisi za serikali na mashirika ya umma yasiyoleta ripoti Barazani. Kwenye sheria yao ya uanzishwaji inayo *room* ya kuleta *annual report* ina *room* ya kuleta *auditing* na *financial report* katika Baraza letu. Lakini *ZIPA* moja wapo yenye sheria ambayo inatakiwa ilete ripoti hiyo lakini tangu kuanza kukumbusha bado haijaleta. Mhe. Mwenyekiti, tunasali na adhana inasomwa si kuwa hatujui muda wa kusali lakini tunakumbushana. Lakini kwanye Baraza Mhe. Dimwa tayari alishakumbusha lakini bado. Sasa niseme tu kama fungu hili nitalizuia la *ZIPA* na sitoliachia mpaka nione basi jinsi gani nimepewa ripoti hii na makatibu mezani muandike, hili nategemea kulizuia kabisa kulichukua fungu langu hili la *ZIPA* mpaka niambiwe kitu gani wanachokifanya.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nataka kujua katika mwaka huu wa fedha ni miradi mingapi ambayo imetekelezwa au ma-*investors* wangapi wameomba na mingapi imefanikiwa na mingapi haijafanikiwa na hiyo iliyokuwa haikufanikiwa kwa kitu gani ambacho hakijafanikiwa, kuna ugumu gani. Nilikuwa nataka kujua Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze, lakini bado *ZIPA* tuna kazi kubwa ya kuitangaza Zanzibar nje ya nchi. Balozi zetu nyingi sana hakuna *brochure* ambazo zinaeleza Zanzibar. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri kupitia taasisi hii kuweka bajeti maalum ya kupita nchi nyingi ili kuona basi utalii na mambo mengine ya *investment* yanakwenda vizurin na mapato mazuri katika serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye *PBZ* kwanza niwapongeze sana kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya, lakini vile vile niwapongeze kwa kushusha riba ya mikopo, sasa wananchi na wafanyabiashara watakuwa na muda mzuri wa kuweza kwenda kukopa na kuweza kuona biashara zinakwenda vizuri. Niwapongeze sana kuwafikiria wanyonge lakini vile vile nataka niwashauri waangalie sheria zao waweze kuiga mfano wa *NMB* kuwakopesha wananchi wa kawaida wenye biashara ndogo ndogo ili waweze nao kufanya biashara za kawaida kuondoa

masharti magumu ambayo wanaweza kuyaweka. Sasa niwashauri hiyo ili kwa sababu tumeona *NMB* imepiga hatua kubwa sana na benki yetu hii ya miaka mingi ipo haina hatua nyingi ambazo zilizopiga, niwashauri hili nataka nishauri tu kuweka masharti nafuu kwa wakopaji wetu wafanyabaishara ili kuona wanakwenda vizuri.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niingie kwenye mfuko wa barabara. Nataka niwapongeze sana kwa kazi kubwa wanazozifanya lakini Mhe. Waziri hapa tulikuwa tuna pesa zetu za tozo mbali mbali ambazo zinatoka. Sasa uniambie tu mipango ya muda mrefu ya Mfuko wa arabara ukoje na je, umepanga vipi kuondosha zile *feeder road* za Mpendae kuweza kuzijenga kwa sababu bado kwenye mamlaka haijapangiwa pesa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka niende kwenye kitabu kikubwa namuomba Mhe. Waziri akamate kitabu kikubwa niangalie kuna ukurasa wa 5 kwenye kitabu hiki kikubwa cha A415 Mamlaka ya Uwekezaji *ZIPA*, katika kiashiria cha idadi ya wawekezaji wa ndani na wa nje walionekana hakuna taarifa yoyote iliyojazwa kwa mwaka 2017/2018 na miaka mengine pia haikujazwa wala haina *target* ya mwakani. Sasa nilikuwa nataka kujua lakini pia ukifanya rejea katika kitabu kikubwa cha bajeti cha mwaka 2017/2018 pia utakuta eneo la *ZIPA* katika kiashiria hiki cha chini hakuna taarifa yoyote iliyojazwa kutokana na umuhimu wa uwekezaji katika ukuaji wa uchumi. Je, kunakosekana kwa taarifa hizo muhimu kwa miaka miwili mfululizo inatoa taswira gani kwa wananchi, nilikuwa nataka kujua kiashiria hiki, hakina mwaka jana hakina mwaka huu lakini hakina *target* ya mwaka 2019/2020, lakini hakina *target* ya 2020/2021. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kujua Mhe. Waziri atakapo kuja aniambie kwa nini viashiria hivi vinakaa hivi au hatuvijui au hatuna takwimu sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka tena twende kwenye ukurasa wa A414 Idara ya Fedha za nje kupitia programu ya Uratibu wa Fedha za Nje, katika kiashiria cha asilimia raslimali ya fedha zilizopatikana kutokana na viashiria washirika wa maendeleo ambayo katika utekelezaji wake kunaonekana kuna asilimia 100. Hii ina maana kuwa fedha hizo zimepatikana kama ilivyotarajiwa bila ya upungufu wowote. Mhe. Mwenyekiti, mimi nikiwa ni Mwenyekiti wa Kamati wa Bajeti nina hofu kidogo na taarifa hizi. Nina hofu na taarifa hizi lakini nina hofu na uhalisia wa takwimu hii kwa kuwa nafahamu moja ya changamoto kubwa za utekelezaji wa bajeti zetu ni upatikanaji wa fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo. Naomba kupatiwa ufafanuzi juu ya takwimu hii lakini pia ningependa kufahamu mikakati ya serikali juu ya kupunguza utegemezi wa bajeti kutoka kwa washirika wa maendeleo ambao fedha zimekuwa hazipatikani kama ilivyotegemewa na hivyo kuzorotesha utekelezaji wa bajeti nzima ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nikiomba hilo Mhe. Waziri atakapokuja aniambie, hapa nitakuwa sina msalie Mtume kidogo, nataka kujua hasa bajeti ya serikali inaweza kutekelezwa vipi. Lakini katika ukurasa huo huo wa A414 Idara ya Fedha za Nje kupitia programu ya Uratibu wa Fedha za Nje katika kiashiria cha huduma ya ufuatiliaji wa raslimali za nje, kuna namba 8 yaani hakuna kiashiria kilichotajwa na badala yake kuna namba 8 tu, lakini katika utekelezaji wa miaka yote napo pia hakuna namba 8. Mhe. Mwenyekiti, kimsingi mimi sijafahamu kiashiria hiki. Je, hizi namba 8 ni asilimia au ni idadi lakini pia nataka kujua tu Mhe. Mwenyekiti, naomba kufahamu kiashiria halisi cha huduma hii ya ufuatiliaji wa raslimali hizo za nje zinazoweza kupatikana.

Mhe. Mwenyekiti, nimesahau kule kwenye *PBZ*. Mhe. Mwenyekiti, *PBZ* inafanya kazi nzuri lakini moja ya *ATM* zake nataka kwanza kuweza kuishauri kuendelea kutoa elimu ya *ATM,* watu wanakaa muda mwingi bila ya kujua lakini iendelee kutoa elimu ya *ATM* pale wanapowapa wa *ATM* watu ili kupunguza msongamano unaokuwa ndani. Lakini jambo jengine *ATM* za Mwanakwerekwe Mhe. Mwenyekiti, zimepitwa na wakati sana na aje niambiwe mna programu gani za kuweza kuzibadilisha *ATM* zile ili kwenda na wakati sasa, zimekuwa zikiguma mara kwa mara lakini utwambie *system* ambayo iliyokuwepo kwa nini ikifika mwisho wa mwezi wananchi wengi wamekuwa wanapata taabu na kadhia kubwa, *system* zimegoma kutokana na je, *system* inazidiwa au uwezo wetu mdogo katika kupanga mipango yetu. Naomba hapa aje aniambie ili niweze kujua kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimesema leo sitokua na michango mingi lakini nasema tu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF).* Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mkurugenzi wa *ZSSF* kwa kazi kubwa ambazo anazozifanya na mimi nilikuwa na *theory* moja kwenye kichwa changu, akinamama hawa tunapowapa nafasi wanafanya kazi nzuri na wanakuwa waaminifu sana. Mhe. Mwenyekiti, leo nilikuwa nimeazimia sana kuja kuona kama kuna ufisadi ambao ulitendeka kwa *ZSSF*. Kwanza kwenye mashine zile za watoto kiwanja cha watoto lakini kwa nyumba hizi, lakini kwa sababu yule ambaye tutamuhukumu siye aliyepewa, nikasema hili niliondoe lakini nichukue fursa hii kumpongeza sana, anafanya kazi nzuri na ninataka nimwambie avute soksi yake juu ili aweze kutekeleza majukumu haya ipasavyo.

Mhe.Mwenyekiti, lakini vile vile niwapongeze sana *ZIC* Bima kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya, lakini pia na kutangaza taasisi yao vizuri ili basi tuweze kuona Zanzibar sasa Bima yetu inaweza kuenea kwa Tanzania Bara hii haikamatwi kule bara kama sukari, hii inaendelea vizuri tu na tunaishukuru kwa matangazo makubwa. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nimesema leo sina mazungumzo mengi lakini kubwa Mhe.Waziri ningekuomba suala la *ZIPA* na uletaji wa ripoti Barazani, hii naomba niikamate na kifungu hiki nitakishikilia barabara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache sana kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mpendae naunga mkono hoja hii kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya bajeti kwa asilimia 95 na asilimia 5 naomba nichukue mpaka nitakapopewa jawabu sahihi. Lakini niwaombe Waheshimiwa wote Wajumbe kupitisha bajeti hii. Kama alivyosema Mhe. Yahya Abdulwakil bajeti hii haina matatizo iko vizuri sana na Mhe. Yahya jambo lako zuri lakini nilipingana na wewe kwa sababu mimi Mwenyekiti wa bajeti huwezi ukanikiuka moja kwa moja. Nikushukuru sana.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushuru Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali na mchangiaji wetu wa mwisho nitampa nafasi Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali: Mhe Mwenyekiti, awali ya yote kwanza naomba napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa pumzi tukafika katika kikao hiki *Alhamdulillah*.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja kuipongeza au kuishukuru bajeti ya Wizara ya Fedha kwa kazi kubwa waliyoifanya. Mhe. Mwenyekiti, kwa kitabu hiki niseme leo Zanzibar tuna historia kwamba katika kitabu hiki inaonesha makusanyo ya pesa kwamba tumefikia sasa Zanzibar kwa usikivu, uvumilivu na busara ya watendaji chini ya Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein, kupitia Wizara ya Fedha na taasisi zake kwamba *Alhamdulillah* ni historia kwa leo Zanzibar kwamba angalau makusanyo yetu ya ndani katika nchi hii tunaweza kuiendesha serikali yetu ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Kwa hivyo hili ni jambo la kihistoria kwa Rais Dkt. Ali Mohamed Shein na watendaji wake wote wa Wizara ya Fedha na taasisi zake kwamba hatuna tegemezi ya kuweza kuiendesha nchi yetu, na nirjee kusema kuna siku alisema Mhe. Rais Mstaafu alipokuwa madarakani Komandoo, narejea kauli yake aliposema "Bora tule muhogo na mashelisheli lakini tuweze kujiamulia mambo yetu wenyewe". (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Fedha pamoja taasisi zake zimefanya kazi kubwa na ninachosema sisi wafanyabiashara pamoja na wananchi tubadilike kulipa kodi, tunahitajiana sote kazi kubwa wanazofanya taasisi zote hizi *ZRB*, *ZIPA* na sehemu zote. Mhe. Mwenyekiti, mimi niende moja kwa moja kuzishauri taasisi hizi za *ZRB, TRA*, *ZIPA* na sehemu zote nyingine zinazohusika na ukusanyaji wa kodi. Mhe. Mwenyekiti, bado kuna haja ya kutoa elimu kwa wafanyabiashara na kutoa elimu kwa wawekezaji kwamba lazima tubadilike.

Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye *ZIPA* tumewekeza wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi lakini inapofika mwaka wa kwenda ku-*renew* leseni tunapata taabu sana wafanyabiashara kwenda kulipia. Kwa hivyo tunakwenda kulipia mbio leseni ya utalii ili mahoteli yetu yaweze kufanyakazi lakini tunawacha *ZIPA* kulipa *reaaliity* ile ya kila mwaka ya kuwezesha ile *ZIPA* kufanya kazi. Sasa mimi niombe Wizara ya Fedha kupitia taasisi hii zikae kwa pamoja *ZRB*, *TRA* na sehemu zote za makusanyo ya kodi waende kwenye *system* moja watizame kampuni gani katika mwaka huu wa fedha haijalipa kodi yake.

Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi sisi tukabembeleza kwa wawekezaji akina Raza wakumbushwe mara nne kwenda kulipa leseni ya dola 500 dola 1000 wakati mtu ameweka pale dola milioni 2 milioni 3. Sasa mimi nasema tufike pahala kwa sababu humu humu ndani ndiyo sisi walalamikaji kwa wananchi kwamba barabara zetu mbovu, hatuna maji lakini pesa hizi si lazima ziingie kwenye mfuko wa Hazina. Kwa hivyo nitoe wito kwa Wizara ya Fedha katika taasisi hizi siyo kila anayepepesuka ni mlevi, ukitaka kumchinja nyani usimtizame uso wake.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze *ZRB* na taasisi nyengine ziige mfano usipolipa na huna hoja maalum ya kucheleweshe kodi, *you pay fifth percent,* huwezi kubembelezwa mtu ume-*invest. S*asa nataka *ZIPA* na wao hakuna haja ya kutoa barua unamkumbusha nani, tunapotaka kutoa mizigo, kuleta mtu utashinda pale siku tatu, utashinda Wizara ya Fedha siku nne. Mimi nafikiri bado kuna haja ya kupata kuongeza mapato yetu, lazima atufatilie mapato. Kwa hivyo nitoe wito kwa taasisi hizi tuwe makini katika suala la leseni kwa sababu utakuta kwamba pesa nyingi zinakuwa zimekwama na hatuwezi kufanya kazi, kama *ZIPA* wanajitegemea wanataka kujiwezesha lakini leseni watu hawalipi. Sasa hili ni jambo muhimu sana kila mtu akiwemo Raza kama hajalipa asipewe huduma wala asisafiri huu ndio ukweli.

Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu ni sikivu sana Dkt. Ali Mohamed Shein ni kiongozi ambaye anaongozana na serikali yake, wamekuwa watu wenye hekma na busara kila kilichotakikana kwa ajili ya Zanzibar kinafanyika. Kwa hivyo mimi nitoe wito kwa wafanyabiashara kwamba katika historia yetu ya Zanzibar Mhe. Mwenyekiti, katika Afrika ya Mashariki na Kati na katika Afrika nzima basi Zanzibar tuna ahuweni sana, viongozi wetu wanatupenda alhamdullilahi, hakuna mtu anayepata hasara. Kwa hivyo hilo lilikuwa ni ombi.

Lakini nitoe wito vile vile kwa *ZRB* tumeona viongozi wengi wanakuja, wafalme wanafikia kwenye mahoteli makubwa makubwa. Lakini kuna hoteli Mhe. Mwenyekiti, ukenda kwenye *rate* unakuta dola mia nne mia tano, lakini hoteli ile ile na mimi ninaijua, inatoza dola elfu tano *swift* na mimi naijua, dola elfu nne. Sasa mimi nimuombe Kamishna wa *ZRB* ni mtu mwenye hekma mwenye busara msikivu amekuwa katika Serikali hii zaidi ya Miongo kama sikosei mitatu, akae na timu yake wafanye utafiti katika mambo ya *return. L*eo Mhe. Mwenyekiti, hoteli za kimataifa hizi tunazo tunazokwenda na sisi wenyewe tunakwenda, keki moja ukiagiza shilingi elfu kumi na tunalipa. Sasa sote tunahitajiana. Serikali inahitajia wafanyabiashara, wafanya biashara wanaihitaji Serikali kwa hivyo sote tunahitajiana katika huduma, sasa lazima tukae namna ya kuongeza mapato.

Kwa sababu nasema tumefikia pazuri lakini lazima tuongeze mapato na mapato haya yanakwenda kwa wananchi. Hivyo mimi nitoe ushauri kwa *ZRB* na taasisi nyengine zikae zitafute na zipo wazi, leo ukenda kwenye mahoteli zinafahamika anakuja mfalme analipa dola laki tatu. Sasa hili lifanywe tathmini waitwe wawekezaji waelezwe kwa njia nzuri ya kupendana, unajua hii kazi ni nzuri Kamishna wa *ZRB* na Kamishna wa *TRA* muwaalike wafanyabiashara muwaweke *breakfast* au chai ya pamoja, kwa sababu ndio utaratibu wa duniani, unawaelimisha mnafahamiana kwa sababu hapa hakuna uadui ni suala ambalo la kuwekeza ili pato liweze kuongezeka.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi niombe taasisi kwa kazi kubwa wanayoifanya *ZRB* na taasisi nyengine. Lakini vile vile nitoe wito Mhe. Mwenyekiti, umefika wakati sasa sote wafanyabisahara lazima tu-*declare* ma-*go down* yetu ili vifahamike vitu vilivyokuwepo, kwa sababu wakati mwengine mizigo kutokana na *ZRB* na ukusanyaji wa kodi sisi wafanyabiashara wajanja huwa tunatoa mizigo usiku. Halafu tukifika hiyo hiyo tunakuja Serikali imefanya kazi gani, Serikali ya Mapinduzi ya nini.

Mhe. Mwenyekiti, mimi jana narudi nyumbani Kibweni gari ya *carry* imepakia tani nne ya nondo Wallahi laadhim zinakwaruza barabara. Sasa mimi hushangaa hii nchi ioo wapi, *carry* halafu sisi humo humo tunakuja tunailamu Serikali, *carry* imepakia tani nne inakwaruza barabara. Mhe. Mwenyekiti, mimi Dubai hivi karibuni nilikata barabara tu ambayo pamoja na wenzangu 30 ina *traffic light* lakini hakuna watu, wallahi tulisombwa sote tukawekwa ndani Mhe. Mwenyekiti, tulikamatwa sote. Sasa lazima tuwe na utamaduni kila mmoja awe na hamu na uchungu wa nchi. Sisi leo tunapakia mizigo magari makubwa, zile nondo tunazikwaruza barabara, barabara ile ikiingia shimo tunakuja hapa kuisema hii Serikali tunailaumu, lakini sisi tumeisaidia nini Serikali Mhe. Mwenyekiti. Jana mimi tena nilitaka kuteremka, dereva wangu akaniambia Raza unaumwa wewe, sukari yako itazidi kupanda, nilihisi uchungu ninakwenda

nyumbani nahisi uchungu nondo imekwaruzika imeanza mjini hakuna hata mwananchi anayeshughulika.

Sasa mimi nitoe wito kwa wananchi, jeshi, vikosi vyote gari zinavyokutwa kama hivi zikamatwe, hatuwezi kukaa Serikali inakusanya pesa na Serikali ya Rais Dkt. Ali Mohamed Shein inajitahidi kutoa huduma, halafu anatoka mtu anakwaruza barabara na nondo. Sasa mimi niombe sana kwamba lazima tuwe na utamaduni wa kusaidiana katika Serikali yetu, leo tunakusanya mapato sasa mapato haya tunataka tuyadhibiti. Lakini tukikusanya mapato hatuwezi kuchukua pakacha ya makaa ukatia maji itakuwa hatwendi, kwa hivyo mimi nitoe wito tu.

Mhe. Mwenyekiti, niombe tu katika Wizara ya Fedha katika suala hili, huko nyuma tulikuwa na utamaduni wa Serikali yetu viongozi kiuchumi, *I am not talking politics*, viongozi wetu wanapotoka nje wakitoka nje kwa ndugu zetu Bara viongozi wana utamaduni kuja Zanzibar kiuchumi. Kwa mfano alikuja Waziri Mkuu wa India mle ndani mlikuwepo suala la biashara Zanzibar India kutusaidia. Historia ya India kwa Zanzibar Mhe. Mwenyekiti, ni sawa sawa Kikwajuni kuuliza Asumini. Kwa hivyo tumekuja tulikuwa na utamaduni lakini leo utamaduni ule siuoni sijui kuna sababu gani, amekuja Rais wa Uturuki amefikia pale na huku kuna mkutano wa pamoja, Uturuki kusaidia Zanzibar. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kiutangulizi tunataka kuwaambia ndugu zetu wa Bara kabla ya April, mwaka 1964 nchi mbili hizi zilikuwa huru na nchi 17 kabla ya uhuru na muungano wetu na utadumu kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu.

Kabla ya Muungano wetu nchi 17 ziliitambua Zanzibar ikiwemo India, China, Marekani, Uingereza, Ghana, Egypt, *Commonwealth countries* ni nchi kumi na saba. Mhe. Mwenyekiti, hichi ndio kitabu ambacho nilikizungumza mwaka 2000 ambapo kero zote za uchumi nilizielezea, kwa bahati nzuri kitabu hichi nilipata baraka ya Mhe. Rais wa Zanzibar kusaini akiwa madarakani Comandoo ambacho nitawasilisha hapa, kitabu hichi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, tukaeni tutizame au tuiambie Wizara ya Fedha tumwambie *Pay Master General* Khamis Mussa hivyo kweli anashindwa kutupa bajeti ndogo ya kumleta kiongozi Zanzibar ili aje tupate neema, tunazungumza uchumi. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi naona suala hili litasaidia sana katika mambo yetu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, la mwisho katika mambo yote yametukwaza katika suala la makusanyo ya pesa. Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mkweli kwamba Tume ya Pamoja ya Fedha imo ndani ya Muungano *page 133* na *page 134*, atanisaidia Mwanasheria Mkuu, imo ndani ya Katiba Tume ya Pamoja ya Fedha. Tume hii ilimalizika mchakato wake wa kuweka sawa mwaka 2006 na Tume hii ingelikuwa imefanya kazi hapa Mhe. Mwenyekiti, unapata kigugumizi. Leo tuna *shares* zetu *Air Tanzania*, *TTCL*, Mashirika yote ya Muungano kwa sababu hatukuwa na Tume ya Pamoja ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, kukosekana Tume ya Pamoja ya Fedha tutakaa siku zote tutalaumiana. Mhe. Mwenyekiti, tokea mwaka 2006 vikao vikawa vinaendelea na vikao Kikatiba havikutani Kikatiba kama mwaka mara nne. Sasa inaelekea wenzetu labda huko watendaji wa chini Bara hawaitaki kwa sababu hii ingelitumalizia matatizo yetu yote ya Muungano. Mimi ushauri wangu Tume ya Pamoja ya Fedha, nimuombe sana Rais John Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar, kule kuna Nyerere mdogo huku kuna Karume

mdogo, Mwenyezi Mungu awape nguvu tufike pahala hii Tume ya Pamoja ya Fedha imo ndani ya Katiba.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar tunaweza kujiendesha kwa mambo mengi lakini tumekuwa tunakosa mgao wetu na mimi naamini wenzetu huku chini hawaitaki, kwa sababu sioni sababu imo ndani ya Katiba na imejadiliwa 2006, ile Tume ingelitolewa hadharani maoni ya watendaji wa pande zote mbili, imekaliwa lakini watu wanakutana mwaka mara moja, mwaka mara mbili, wanakutana masaa mawili imekwisha. Mhe. Mwenyekiti, tatizo letu katika kuudumisha Muungano wetu Wazanzibari tunaupenda Muungano tutaendelea kuupenda, lakini ninachotaka kusema kuwaambia ndugu zetu tujadiliane, tuvumiliane na tuheshimiane nchi mbili huru zimeungana.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mtu ambae kidogo alhamdulillahi nimelelewa ndani ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar na kufika hapa kwa sababu ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Tatizo ni dogo, viongozi hawa wawili Mhe. Mwenyekiti, wakijifungia masaa mawili, Wallahi kama zawadi nzuri anaweza kumpa Rais Magufuli Dkt. Shein basi ile Tume ya Pamoja ya Fedha, itatuondoshea matatizo yote katika nchi hii. Lakini tutakuwa tunasumbuka siku zote, kuna mafao yetu ya *four percent*, kuna mafao yetu ndani ya muungano, kuna mafao yetu ndani ya Afrika ya Mashariki, kuna mafao yetu kwanye Benk Kuu, mambo mengi leo ndio maana nikasema…

Mhe. Mwenyekiti: Malizia Mheshimiwa.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, huko nyuma tulikuwa na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, kati kati wenzetu walipoona sasa tunajitanua wakaiongeza Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, Ushirikiano wa Kimataifa Muungano. Sasa katika uchumi, *We have any economic*, naomba nimalizie Mheshimiwa sijakusikia naomba unisamehe.

Lakini Mhe.Mwenyekiti, mimi niombe sana leo humu kwamba nimuombe na Kiongozi wa Baraza Mzee wangu baba yangu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwamba hii Tume ya Pamoja ya Fedha Wallahi Mheshimiwa siku moja tutamaliza matatizo yote hayo.

Mhe. Mwenyekiti, niunge mkono Wizara hii niunge mkono watendaji wote wa Wizara hii na Serikali kwa jumla kwa kazi nzuri na kwa niaba ya wananchi wa Uzini, kwa niaba yangu mimi naunga mkono kwa asilimia mia bajeti hii na Mwenyezi Mungu atatujaalia tuweze kufikisha hapo tutakapofika Mungu ibariki Zanzibar, Mungu ibariki Tanzania ahsante sana.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ninatoa kitabu hiki iwe kama ni kumbu kumbu ambayo imeelezea mambo yote ambayo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Komandoo Dkt. Salmin Amour Juma ambaye ametia saini akiwa madarakani, ndio maana ya kusema kwamba hichi kitabu kimepewa baraka baada ya mimi kuandika na naendelea kuandika kitabu chengine Mhe. Mwenyekiti, nini nimeifanyia Zanzibar na changamoto iliyokuwepo Zanzibar, naomba kuwasilisha Mheshimiwa kwa Waziri wa Fedha ili ikamsaidie hii. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako na kitabu kimepokelewa. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa Wajumbe kabla sijampa Mhe. Waziri naomba nimuite Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii niweze kuchangia machache katika Wizara yetu hii ya Fedha na Mipango. Kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima, lakini pia vile vile kuwa salama katika Baraza letu hili kuweza kufikia nng'we hii tuliyobakia hapa.

Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kuiweka nchi yetu na amani na tukaweza kutekeleza majukumu yetu, bila ya amani haya yote yasingekuwepo. Lakini sasa niendelee katika mchangio wangu nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wake wote waliotaharisha kitabu hichi na yeye akawasilisha kwa umakini kabisa. Kwa kweli hichi kitabu kimesheheni mambo mengi na muhimu sana lakini kusimamia na kufanyiwa kazi ni jambo muhimu sana na nimpongeze sana, kazi aliyokuwa nayo Wizara ya Fedha Waziri wetu huyu ni kubwa sana na nimpongeze sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwamba hakukosea, alisadifu sana kuona kwamba amempa mtu ambaye kuwa na yeye ana uchungu wa nchi hii na kusimamia vyema Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika kuhakikisha mapato na matumizi yanakwend vizuri mpaka Zanzibar ikaweza kupiga hatua nzuri nzuri katika suala la mapato.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tumepiga hatua nzuri sana lakini pia hili lilikuja kutokana na mashirikiano ya Baraza la Tisa, nasema hivyo tuna nafasi ya kujivunia na kujipongeza. Baraza la Tisa nalo limesaidia sana kuibua sehemu mbali mbali za mapato ambayo kuwa yalikuwa yamefunikwa funikwa, lakini Baraza la Tisa hili lililofunguliwa rasmi na Mhe. Rais limeweza kunyanyua uchumi wetu Zanzibar na kuona kwamba leo tupo pazuri.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo bado juhudi zinahitajika kwa Mhe. Waziri na watendaji wake kuzuia ile mianya ambayo kuwa ikipoteza fedha za Serikali, tujaribu kuizuia sana ile ili tuweze kupiga hatua sana. Naomba sana Waziri aendelee kujipanga vyema kuona kamba mapato hayavuji.

Sasa niende katika suala zima la mapato ya *TRA.* Namuomba sana Mhe. Waziri, suala la mapato yanayotokana na *TRA* Zanzibar bado kuna watu wanayapotosha. Sisi tunasema mapato yanabakia Zanzibar kwa ajili ya Serikali ya Zanzibar, lakini kuna watu bado wanapotosha kusema kwamba mapato ya *TRA* yanatiwa mkobani yanapitia uwanja wa ndege, yanapita *custom.* Ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atoe ufafanuzi suala zima la mapato yaliyokusanywa na *TRA,* sisi tunaelewa kwamba ni wakala ambaye kuwa anawakilisha Zanzibar katika kukusanya mapato haya.
Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika program ya ujenzi wa ofisi za Serikali ukurasa wa 35. Wizara hii ilipangiwa kutumia bilioni 5.57 lakini hadi mwezi wa Machi ilipata bilioi 4.02 sawa sawa na asilimia 2, niseme kwamba niipongeze sana Serikali katika suala zima la maendeleo kama haya hapa kwa ujenzi wa ofisi za Serikali, jambo ambalo kuwa mara nyingi sana humu Barazani tulikuwa tunalishauri, kwa sababu tumeona kwamba Serikali inapoteza pesa nyingi kwa ajili ya kukodi nyumba za watu binafsi kuendesha shughuli za Serikali. Lakini hii ni

hatua nzuri sana iliyofikiwa kuona kwamba kule Pemba majengo pacha yapo yanaendelea vizuri sana na Serikali ikakubali kutoa asilimia kubwa ya fedha ambayo kuwa imepanga, hilo ni jambo zuri sana na linafaa kuendelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pamoja na kazi nzuri iliyofanywa kuna jambo zima naomba atakapokuja Mhe. Waziri anieleze suala zima la Jengo la Wizara ya Kazi, hili jengo limeelezwa hapa kidogo lakini litamalizika lini nalo naona linakwenda likisuasua sana, jengo la Wizara ya Kazi na Uwezeshaji amba lipo Mwanakwerekwe. Pia niipongeze Serikali kwa kumaliza malipo ya mwisho ambayo yalikuwa yanadaiwa na mkandarasi wa jengo la Katiba na Sheria, sasa liko huru halina madeni yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa ambayo Serikali inafanya kuna watu ambao kuwa bado anarudisha nyuma maendeleo haya, mimi napenda sana Waziri atakapokuja atueleze juu ya mkandarasi ambaye kuwa alijenga jengo la Wizara ya Fedha Pemba na baadae ikawa jengo lile halikufaa ni bovu, hatujui hatua gani ambayo imechukuliwa. Naomba sana atakapokuja atueleze hatua gani zilizochukuliwa dhidi ya mkandarasi yule ili kuona kwamba fedha za wananchi hazikupotea bure. Hili nazungumza kabisa sina nia ya kuzuia bajeti lakini pengine Waziri asitoe maelezo, kwa hivyo kama hakutoa maelezo nitazuia kifungu cha PF 0104 mpaka tupate maelezo, hii PF 0104 Uendeshaji wa Wizara ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, niende suala zima la mradi wa kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge Tanzania *MKURABITA.* Huu mradi ulipangiwa Tanzania TZ. Shs. Milioni 400 lakini zikapatikana TZ.Shs. Milioni 376 ni hatua nzuri sana. Katika Wilaya tano zilizopatiwa uelewa ni zipi za Unguja na Pemba tuweze kuzielewa, hapa imeeleza tu wamepata Wilaya tano katika ulewa wa suala zima la *MKURABITA*, sijui ni Wilaya zipi, maana Wilaya ziko zaidi ya tano tungependa kuzielewa ili tuweze kuzifuatilia hatua gani zipo na zinaendelea, nini matokeo yake lakini baada ya kupewa uelewa, nini maeneo ya kupewa uelewa wa *MKURABITA* wananchi wametumia vipi fursa ya rasilimali za biashara na ardhi zilizopo katika kujikwamua na umasikini kama wamefanya uelewa na wanafuatilia basi ni vyema atueleze tuone matokeo yake, ni yepi ili lile lengo lililokusudiwa lifikie.

Lakini pia vile vile Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nataka nieleze kwamba katika Jimbo langu la Mgogoni, katika Shehia ya Kiungoni ipo ofisi hii ya MKURABITA, tulishiriki katika kuifungua pale na alikuwa mgeni rasmi Mhe. Makame Mnyaa, Waziri wa Mawasiliano. Kwa hivyo je, katika vitendea kazi alivyosema vimepatikana ofisi hii imepatiwa, atakapokuja atueleze kwamba nayo ipo kwa sababu moja ya matatizo yaliyokuwepo ni vitendea kazi katika ofisi hii, ipo katika Shehia ya Kiungoni.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika programu ndogo ya usimamizi wa sekta fedha, mapato yatokanayo na kodi. Hii niwapongeze sana Mhe. Waziri kwa kuona kwamba mapato yanaendelea kupatikana vizuri, lakini kuna suala zima alilolieleza hapa kufanya vikao na wadau mbali mbali kwa ajili kujadili mfumo bora wa ukusanyaji wa mapato kwa mwaka 2018/19. Hili ni jambo zuri sana kwa sababu tumeona kwamba kila uchao unaokuja wanalalamika hukusu kodi. Sasa hizi ni vyema kukaa pamoja tukuona kwamba jambo hili tunaliendesha vipi baada ya

kila siku tunapiga kelele kwamba tunatozwa kodi mara mbili kwa jambo hilo hilo moja haikubaliki.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tukikaa pamoja na kujadili mfumo gani ambao kwamba utatusaidia ni jambo zuri sana, lakini tuondoe kasoro ambazo kuwa zipo moja kwa moja. Lakini pia vile vile ili kuona kwamba kodi sinakusanywa vizuri ule mfumo wa kutumia *EFB* ni muhimu sana. *EFB* ni muhimu sana tunaona wenzetu ambao kuwa wanautumia na mafanikio waliyopata, huwezi kwenda Tanzania Bara hata ukanunua kilo moja ya nyama kwenye *butcher* utapewa risiti.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja niliwahi kumuona mtu anashangaa, kenda kununua nyama pale anapewa risiti, kwa sababu wenzetu walivyoupokea lakini leo hapa petu unakwenda unanunua vitu hata milioni nzima mpaka udai risiti kwa nini mtu adai risiti, kutoa risiti ni wajibu wa muuzaji, leo ukenda vituoni hata ukanunua mafuta ya laki mbili, tatu mpaka udai risiti. Naomba hili jambo lisimamiwe vizuri kuona kwamba linatekelezwa ipasavyo ili tuone kwamba mapato yetu hayapotei, kwa sababu mfumo huu ni mzuri hata kama ule ukilinganisha na ule wa zamani kama ulikuwa unaweza kumsaidia mtu wa rafiki yako hapa huwezi kumsaidia, ila uweze kupata fedha nyengine katika mfuko wa serikali. Mhe Mwenyekiti, ni mfano uliohai juzi nilipoteza kadi yangu ya gari ya karibuni nikataka nipate msaada lakini nikaambia haiwezekani lazima nilipe. Maana ukiacha mtandao ukiweka pale lazima inakudai fedha. Nilifanya hivyo, hivyo nikaona kwamba hapa ni njia nzuri ya kuzuia mapato, njia ya mashine na njia elektroniki hizi tunazozitumia ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende suala zima la usimamizi wa deni ya taifa. Hatua ya deni la taifa mpaka sasa hivi ambao kuwa wameeleza deni lote Shilingi bilioni 519 , lakini deni la ndani ni shilingi bilioni 158.3. Ninataka kujua kati ya hili deni la ndani ambao kuwa nina mambo ya viinua mgogo ya wastafu na mambo mengine mbali mbali, lakini je, lile deni ambalo kuwa Mabaraza yetu ya miji ya Pemba, Chake Chake, Wete na Mkoani ambao ilikuwa inadai huu ni mwaka karibu wan nne. Je, limo katika deni hii, atakapokuja anieleze kwa sababu bado wananchi hawa wanatulalamikia kuona kwamba deni lao hili la Waziri Waziri wa Kazi pale alipoeleza kwamba deni hili kweli la marekebisho ya mishahara watu hao hadi leo hawajalipwa, naomba sana walione kwamba ni muhimu sana. Lakini suala zima la malalamiko ya kiinua mgongo. Kiinua mgongo kwa mfumo sheria tulioipitisha hapa kwa kweli inalalamikiwa. Sasa sijui Mwanasheria Mkuu alilifanyia kazi vipi suala hili. Naomba sana Waziri atakapokuja nalo atutolee maelezo suala zima la Sheria ya Kiinua Mgongo wameshirikiana vipi na Mwanasheria Mkuu kuona kwamba kiinua mgongo bado kinabaki kwa mwananchi mwenyewe peke yake, bila ya kufanyiwa marekebisho yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu waliopita hapa waliwahi kuchangia suala hili na mimi niliwahi kulisema kabla ya bajeti hii ya Wizara ya Fedha kwamba hii sheria kama tuliitunga sisi, lakini bado sio msahafu tuweze kuifanyia marekebisho tunaona haitufai, kiasi baada kama miaka mitano au sita mbele ndio iweze kutumika. Naomba tena kwa kupitia bajeti hii kwa sababu inashughulikia pia na masuala ya kiinua mgongo katika masuala ya Mfuko Mkuu wa Serikali basi na hii sheria bado naomba tuilete hapa ili tuweze kuifanyia marekebisho kuona watu wanafaidika kabla hawajarithiwa. Maana mtu kila mmoja anapanga katika kiinua mgongo

nitafanya nini. Wengi wamepanga wakimaliza wapate wakanye ibada ya Hijja. Kwa hivyo wafanye jambo hilo kwa uzuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti niende katika utekelezaji wa bajeti ya taasisi...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. malizia.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Nam!

Mhe. Mwenyekiti: Naomba umalizie.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Zinazosimamiwa na Wizara ya Fedha ambayo kuwa ni *ZRB*, Mfuko wa Barabara, *ZSSF*, Bima, *PBZ* na *ZIPA*.

Kwanza nizipongeze sana taasisi hizi kwa jinsi gani zinavyochangia katika pato la serikali, lakini pia kwa huduma ambazo zinatoa katika jamii. Kwa kweli zinasaidia pamoja na majukumu yake lakini mfano kama *ZSSF*, Bima, *PBZ* hizo zote zinasaidia katika jamii kuona kwamba zinaongeza nguvu, kwa sababu wao ni sehemu ya wananchi hawa, lakini niwapongeze zaidi Bima kwa pale ambapo kuwa wanalipa mafao yao yale ambayo yamekaliwa na mkataba na wananchi kuona kwamba sasa hivi Bima inakubalika. Zamani ulikuwa ukimwambia mtu kata Bima kamili anaona ni kazi bure, lakini kutokana na mtindo huu ambao kuwa asilimia kubwa sana ya madai yameshalipwa, kwa kweli Bima inapata wateja wengi zaidi. Naomba iendelee zaidi ili wasicheleweshe wazidi kukubalika Tanzania nzima. Niombe sana lakini *PBZ* pia vile vile nao ni watu ambao wamejitahi katika kuona kwamba huduma zao zinaendelea pamoja na kasoro mbali mbali. Hizi karoso zilizopo wamalizie kuziweka sawa lakini pia kuona kwamba huduma za benki katika Wilaya ya Micheweni kwenye maeneo huru zinapelekwa, bado suala hili halijakaa vizuri. Naomba sana Benki ya *PBZ* itoe huduma zake kule ili waweze wananchi kufaidika, pesa nyingi zinabaki majumbani watu wanapata matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo niunge mkono hoja lakini baada ya maelezo hayo ambayo kuwa nimesema kwamba Mhe. Waziri akija atupe maelezo tuweze kuona kwamba jinsi gani alivyotekeleza mambo hayo.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa fursa hii naunga mkono hotuba hii asilimia tisini na nane, hizi mbili mpaka atakapokuja kutoa maelezo sina nia ya kuzuia lakini lipate maelezo. Ahsante sana Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Shehe Hamad Mattar. Waheshimiwa Wajumbe kabla sijampisha Mhe. Waziri nimeomba na Waheshimiwa watatu dakika tano, acha niwaruhusu Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame dakika tano na Mhe. Hamza Hassan Juma dakika tano na Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboyo ameniomba dakika tano na yeye atoe maelezo.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kutupatia muda huo mchache na naamini sitokuangusha nitajitahidi niende moja kwa kwenye azma hiyo niliyokusudia.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri sana na ambayo ipo moja kwa moja, yaani *straight forward* na tumemfahamu vizuri sana malengo ya wizara, kuna mambo madogo madogo tu tunataka tukazie ili kuweka mambo vizuri sana huko katika majimbo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kubwa nililonalo mimi kwenye ukurasa wa 49 wa hotuba ya Mhe. Waziri anapozungumzia Mamlaka ya Uwekezaji na Uendeshaji Vitega Uchumi (*ZIPA*). Mara nyingi sana Mhe. Waziri na hata Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alipofanya ziara Jimbo la Dimani katika mkutano wetu wa majumuisho alilipata suala la ardhi ya wananchi kwa upande wa wananchi wa Fumba na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alilichukua na akasema atakaa na *ZIPA* na Wizara ya Ardhi kulipatia ufumbuzi, lakini leo mwaka umeshakatika, lile suala bado halijakaa sawa. Mhe. Mwenyekiti, wananchi wameitikia azma ya serikali ya kuifanya *Fumba Satellite City* na linakwenda vizuri hakuna matatizo yoyote. Lakini tunaomba sasa wale wananchi ambao wame-*risk* wametoa ardhi yao ya kulima na makaazi, sasa wafikiriwe na wao sehemu ya makaazi kwa kutengewa maeneo yao ama kupimwa, yaani waruhusiwe na wao maeneo yetu haya ya kujenga, waendelee na shughuli zao, wasiwe na matatizo. Hili tumeshalileta serikali lakini Mhe. Mwenyekiti, naona bado halijakaa sawa. Tunaomba sana serikali hii tuendelee vizuri na mwekezaji wetu, watu wote wamefurahi tunakwenda vizuri na matunda tumeanza kuyaona.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haraka haraka naomba nende kwenye mradi wa *ZSSF* ukurasa wa 45. Tunaupongeza sana mradi wa ma-*blocks* zile kubwa zilijengwa pale kama 9 na ushei hivi ziweka vizuri, napongeza sana ile kazi nzuri inayofanywa. Kubwa Mhe. Mwenyekiti, nataka kuwaomba *ZSSF* wafikirie suala la njia, suala la barabara fikiria sasa hivi kuja Chukwani huku *congestion* ya magari, sasa seuze ma-*blocks* yale yakimalizima, tufikirie wananchi wataingiaje kwenye majumba yake na watatokaje. Kwa hivyo nawashauri sana wawaze suala la utanuzi au ufunguzi wa barabara. Lazima watengeneze barabara nyengine ambayo itaunga kwenye *main-road* ya kwenda *Airport,* yaani wafikirie tu kwa vyovyote utanuzi wa barabara kwa barabara hizi zilizopo nafikiri tutaleta matatizo. Mheshimiwa napongeza sana kwa mradi ule utatusaidia.

Mheshimiwa nna pointi mbili tu, iliyobaki nyengine ni suala la usajili wa wakandarasi kwenye jadweli la *page* 75, makadirio ya mapato yatakayokusanywa na Wizara ya Fedha kwa mpango kwa mwaka 2018/2019. Kuna usajili wa wakandarasi na nyaraka za zabuni *item* ya 14 imeonesha kuwa makadirio ya mwaka 2017/2018 ni shilingi 50 milioni. Kwa mwaka huu wa fedha hakuna matarajio yoyote ya uchangiaji ya wakandarasi. Je, hawa wakandarasi hawatochangia au kuna tatizo gani. Ongezeko la bajeti naona kuna ziro hapa, fine kama ndio *figure* ile ile ielezwe lakini pana *blank* pale pawazi. Sasa hilo Mheshimiwa ningeliweka sawa.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako nime-*note* kazi nzuri sana inayofanywa na Wizara yetu hasa ya Fedha kwenye suala zima la programu ndogo ya ukaguzi wa ndani wa hesabu, tunafurahia sana kazi hiyo na kwa kweli ikifanywa vizuri itaondosha matatizo madogo madogo hata itamsaidia kazi Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye yeye kama *external examiner* anakuja kukagua baada ya wakaguzi wa ndani. Kama ukaguzi wa ndani haufanywi vizuri, kwa hivyo tuna-*create* matatizo wenyewe ndani ya wizara kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, kilichonisikitisha kwamba hii programu nzuri sana lakini asilimia iliyotengewa kipindi kilichopita, pesa walizopatiwa ni asilimia kumi na nne tu ipo kwenye ukurasa wa kumi na mbili, lakini zama malengo yao Mheshimiwa kayataja hapa kwa programu hii yapo malengo kama sita, lakini kubwa zaidi ambalo lime-*strike* ni la tatu anasema wakaguzi wa ndani mia moja kumi na sita wamepatiwa mafunzo ya ukaguzi wa ndani pamoja na uandishi wa ripoti za ukaguzi, *very good* hiyo ni nzuri sana. Lakini sana kama bajeti unawapa asilimia kumi na nne, wakaguzi hao muwafudishe mia moja na kumi na sita watafanya kazi gani. Kwa hivyo ningeomba wenyewe wizara ndani ya keki yao, hili suala la ukaguzi wa ndani walitilie manani sana, ni suala la msingi litaongeza ufanisi katika serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na *observation* ndogo hizo nne tu, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja na nampongeza sana Mhe. Waziri.

Ahsante Mwenyekiti nakushukuru.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Mwinyihaji Makame kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Hamza Hassan Juma dakika tano atafuatiwa na Mhe. Waziri Dkt. Sira Ubwa Mamboya naye dakika tano.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyekiti ndio maana nikawa nakupenda sana kwa sababu nikiomba napata. Mhe. Mwenyekiti, kutokana na muda nimepewa dakika tano, nampongeza Mhe. Waziri kuanzia yeye mpaka mfagiaji katika wizara hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka niende moja kwa moja kwa ushauri Mfuko wa Barabara. Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Barabara mimi nawapongeza sana kwa kuweza kuzitunza vizuri fedha ambazo zinazokusanywa kwa ajili ya Mfuko wa Barabara. Lakini nina ushauri na ushauri wangu ni kwamba wakati wa kutoa pesa hizi kupeleka Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara, urasimu unakuwa mkubwa sana. Maana yake wakati mwengine mpaka wanawaambia viraka vingapi mnataka kuziba. Sasa kwa kweli nikisema hivyo nadhani mtakuwa mmenielewa kwa sababu naokoa muda.

Lakini jengine Mfuko wa Barabara safari hii pesa zimebakia nyingi sana hazikuweza kutumika zinakuwa *carry forward* kwa mwaka ujao. Hii katika mazingira ya kawaida mtu hawezi kuamini mashimo na mahandaki ya barabara tuliokuwa nayo na barabara zetu za ndani *(feeder road)* nyingi zinahitaji kujengwa hazijajengwa mpaka leo, lakini pesa zipo pesa zinarudi. Mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti, kwamba fedha zitumike ili ziweze kufanya kazi ambayo iliyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo lililokuwepo Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara vifaa vyao vingi vibovu. Kwa nini tusitumie fedha za Mfuko wa Barabara tukawanunulia vifaa ili wafanye kazi kwa haraka haraka. Sasa Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja basi alau anisaidie ufafanuzi katika haya maelezo niliyoyatoa kwamba baada ya kuziweka pesa zikabakia, kwa nini tusiwanunulie vifaa *UUB* ili wakaweza kufanyakazi kwa haraka katika maeneo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nakuja katika suala la MKURABITA. Mimi nawapongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo mradi huu hata Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaufanya. Mhe. Mwenyekiti, tatizo tulilokuwa nalo Zanzibar huu MKURABITA umo katika maandishi lakini wananchi hawafaidiki nao. Mhe. Mwenyekiti, MKURABITA maana yake ni Kurasimisha Raslimali za wananchi ili ziwasaidie katika uchumi. Leo Mhe. Mwenyekiti, kuna wananchi wengi wanalalamika hata juzi kwenye hotuba yetu katika Wizara ya Ardhi kuna wananchi wa Makangale kule, ardhi tayari imeshapimwa mpaka leo wao wanashindwa kupewa hati wakaweza kufanyia mambo yao mengine.

Mhe. Mwenyekiti, ardhi ni mali, ardhi unaweza ukenda benki ukakopa pesa ukaweza kuekeza. Leo hawa wawekezaji wote wanaokuja hapa kwenye mahoteli, hawa wanakuja wakishapewa *lease* ndio anakwenda benki anakwenda kuchukuwa pesa anafanya mradi wake. Leo wananchi wetu wengi wana maeneo yao wanashindwa kupimiwa na wengine wameshapimiwa lakini hati zao hawapewi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie haraka haraka nakuja katika suala zima la *PBZ*. Kwanza na mimi natoa pongezi kwamba mabenki sasa hivi yanatupunguzia riba. Sasa nilikuwa namuuliza Mhe. Waziri sisi wengine ni wakopaji wakubwa tena maarufu. Nataka niulize. Je, katika ile riba ambayo itakayopunguzwa sisi tutafaidika vipi. Maana yake kama tutafaidika tuweze kwenda kukopa tena. Mhe. Mwenyekiti, hili nilikuwa naomba jawabu Mhe. Waziri atakapokuja aweze kunipa ufafanuzi.(*Makofi*)

Lakini la mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala zima la madeni. Mimi kwanza nakushukuru sana Mhe. Waziri kwa usikuvu wako, kuna wananchi ambao walikuwa wanadai ndani ya serikali wamekaa kwa muda mrefu zaidi ya miaka mitatu, tumeleta kilio chao umekubali kuwalipa. Lakini nilikuwa na ombi Mhe. Waziri samahani kidogo nusu dakika kwa sababu waziri kidogo anashughulishwa pale, kwa sababu hili ni ombi maalum. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nilikuwa na ombi moja hawa wameanza kulipwa haya madeni lakini tatizo haya madeni wanalipwa wanakatwa na *VAT*. Mheshimiwa mtu pesa imekaa serikalini miaka mitatu, pesa ile kama kaikopa benki basi ile riba ya benki tayari imeshaongezeka karibu mara mbili. Nilikuwa naomba sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa pesa hii imekaa serikalini muda mrefu hii *VAT* waiondoe waje wakate katika malipo mengine ambayo yatafanywa, lakini kwa sasa hivi kuwakata *VAT* kwa kweli hawa wananchi tutakuwa tunawaonea na kwa kweli tutakuwa hatuwasaidii.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyejkiti, naomba sana ule ushauri ambao ninaoutoa kila siku *ZIPA* yale maeneo ya uwekezaji, tuweke maeneo maalum kwa ajili ya kujenga Hoteli za *Five Star*. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi wawekezaji wetu mtu anakuja anaweka uwekezaji mkubwa, *Five Star Hotel* pembeni yake unakikuta kuna kichuchugu, kuna vibanda vibanda vya makuti, tunakwenda wapi. Leo kweli mtalii mwenye pesa yake daraja la kwanza, mtu katoka huko ana *insurance* ile *insurance* yake tu peke yake si chini ya dola 10,000 kwa mwezi, leo ukamuweke katika Hoteli ya *Five Star* halafu pembeni kuna vibanda vibanda vya makuti, tunakwenda wapi. *ZIPA* naomba sana mshirikiane na Wizara ya Ardhi, tuhakikishe uchumi wetu na utalii, tunalinda utalii wetu na tuwe na mpango mkakati kwa ajili ya uwekezaji huo.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi hii kuweza kuchangia bajeti hii. Lakini pia Mhe. Waziri atakapokuja anambia je, *PBZ*, *Visa card* tutapata lini. Sasa hivi tunahangaika tuna watoto wanahangaika na maisha, wengine wanasoma leo ukitaka kumlipia mtoto inabidi lazima uwende *CRDB* na sehemu nyengine. *Why PBZ*, Benki kubwa *giant* hawana *visa card*.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono asilimia mia moja na mimi naunga mkono hoja ya Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil na napingana na hoja ya Mhe. Mohammed Said Mohamme kwamba bajeti hii tusiiunge mkono. Hoja ya bajeti hii iungwe mkono kwa asilimia zote, ahsante sana.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hamza Hassan Juma kwa mchango wako, lakini umenishukuru kuwa ukiomba nakupa na Wajumbe wote wakiomba nawapa lakini mchango wa hoja za serikali. Mhe. Hamza ninakujibu hoja yako, umesema ukiomba nakupa lakini Waheshimiwa Wajumbe wote wakiomba nawapa nikiwa hapa kwenye Kiti. Hoja za Serikali wakitaka kuzichangia ndio ninazowapa. *(Vicheko/Makofi)*

Nakushukuru Mhe. Hamza Hassan Juma, sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti**,** kwa kukuomba na mimi ukanipa. Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kutaka kutoa ufafanuzi wa jambo moja dogo tu ambalo limezungumzwa hapa na baadhi ya waliochangia mada.

Mhe. Mwenyekiti, hapa imeguswa sehemu moja ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji inayoitwa *Zanzibar Maritime Authority (ZMA).* Huu ni Wakala ulioko chini ya Wizara ambayo mimi naifanyia kazi na ni kweli ni Wakala ambao unatia fedha nyingi za kigeni katika Wizara yetu na ina mchango mkubwa katika Wizara ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, Wakala huu umezungumzwa kwamba Ofisi yake ya Dubai imefungwa. Kwa hivyo wanataka kufahamu ni mchango gani unaokwenda katika Wizara hii. Mimi kwanza nilikuwa nataka niseme kwamba Wakala huu Afisi yake Makao Makuu yake yako Zanzibar na huko Dubai ni tawi tu la biashara. Hivyo hapa Zanzibar Wakala huu bado upo na unafanyakazi zake vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kisa cha kufungwa tawi liliopo Dubai. Ninafikiri niliwahi kujibu swali hapa ambalo liliulizwa kwa nini Tawi la Dubai lilifungwa na nikatoa maelezo, ningependa kurudia maelezo yale yale niliyoyatoa kama nilivyojibu swali.

Tawi la Dubai ilibidi lifungwe kwa sababu kazi iliyokuwa inafanywa ni kusajili meli za nje na inatoa bendera ya Tanzania katika kusafiri kwake katika kazi zake. Bendera ya Tanzania ni bendera ya nchi yetu Tanzania Bara na Zanzibar. Kwa hivyo meli yoyote itakayofanya kosa katika yale mambo ambayo haikupewa ruhusa kufanya, basi kwa utaratibu uliowekwa meli ile inakuwa inafutiwa usajili. Sasa inategemea na kosa likoje lakini kosa lililosababisha mpaka

kufikia hivi tulipofikia, kwamba kuna meli ambazo zimepewa usajili na zinapeperusha bendera ya Tanzania lakini zinafanya mambo ambayo hayakukubalika. Mambo ambayo hayakubaliki ni kubeba silaha pamoja na kubeba unga, ambapo ninanukuu kwa maneno mengine.

Sasa meli ambayo iliyokamatwa ikiwa ina shehena ya unga ambapo ilikuwa imezificha katika baadhi ya vitu ambavyo vilivyokuwa vimebebwa, baada ya kukamatwa ndipo Mhe. Rais wa Tanzania kwa mamlaka aliyonayo alikataza kwamba Shirika hili lisifanye kazi na lifungwe mara moja. Mhe. Mwenyekiti, na lilifungwa mara moja kwa sababu anayo mamlaka kwa sababu Tanzania ni Zanzibar pamoja na Tanzania Bara. Kwa hivyo bila ya ubishi hilo lilitekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hata hivyo baada ya kufanyika hivyo kulikuwa kuna mazungumzo ambayo yaliyokuwa yamefanyika baina ya Tanzania Bara na Visiwani kuieleza kadhia hii na kuna baadhi ya meli ambazo bado zipo nyingi zilikuwa zimesajiliwa wakati huo ilikuwa kama mia tatu na kitu na zile zilikuwa zinaendelea na shughuli zake. Lakini zinapomaliza muda wake nazo hatujazisajili kwa mara nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kukieleza hapa kwamba mtu anaposema ilikuwa hii *ZMA* inachangia mapato mengi. Ni kweli lakini linapotokea suala kama hili inabidi kwa vyovyote vile tusikilize maamuzi ya nchi yanavyoendelea. Kamati iliundwa baina ya watu wa Tanzania Bara Serikali ya SMT pamoja na watu wa Tanzania Zanzibar Serikali ya SMZ na majadiliano bado yanaendelea. Haina maana kwamba *ZMA* haifanyi kazi, bado inafanya kazi na Afisi ya Zanzibar ipo. Moja katika makubaliano yaliyofikiwa kwamba tulifunge lile Tawi la Dubai na tumeshalifunga *officially*, kwa hivyo itabakia *ZMA* inafanya kazi hapa Zanzibar katika Afisi yake Makao Makuu Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kufanya hivyo haikuwa kosa ni suala la kulinda heshima ya nchi yetu. Baada ya kufungiwa pia kuna na meli nyengine imeshakamatwa na unga katika hizo hizo ambazo zimesajiliwa. Sisi kama Watanzania hatutoweza kuvumilia hilo, kuvunjiwa heshima nchi yetu, tutazifungia meli zote ambazo zitafanya hivyo na tutakapokamilisha taratibu zote, bila shaka zitafunguliwa, lakini masharti yatakuwa hayo. Tutabadilisha Sheria zetu ili sasa meli yoyote itakayokamatwa na unga iweze kupewa stahiki inayolingana na kile ilichokifanya, sio tu kuifungia pia kuipandisha Mahakamani kwa kuivunjia heshima Tanzania.

Baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Sasa naomba nimwite mtoa hoja Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. *(Makofi)*

MICHANGO YA MAANDISHI

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima napenda kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa umakini wa kumpa uongozi wa wizara hii Katibu Mkuu Mr. Khamis Mussa Omar na watendaji wake wa Wizara ya Fedha na Mipango.

Aidha, napenda kuwashawishi wajumbe wote kuunga mkono bajeti hii ili ifanyiwe kazi. Kwa sababu laiti kama wasingefanya vizuri tusingeweza kutoa huduma muhimu katika jamii kama Pensheni ya Wazee, Elimu Bure, Matibabu Bure na jitihada ya kusimamia miundombinu ya barabara, Usimamizi wa Mikataba ya Utalii na kadhalika kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja na niwaombe wajumbe wafanye hivyo ili wote tubarikiwe.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana tena leo hii tukiendelea katika Kikao chetu cha Bajeti na kwa mara hii tunachangia bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa jinsi ulivyokiendesha Kikao hichi. Lakini pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote waliopata fursa ya kuchangia wale waliotupongeza tunapokea pongezi zao, lakini vile vile wale waliotaka baadhi ya maeneo wapate ufafanuzi sasa niko hapa kutoa ufafanuzi huo kwa Waheshimiwa Wajumbe.

Lakini pia nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo kwa mchango wao mkubwa sana walioutoa katika hotuba hii kushauri, maoni na maelekezo waliyotoa kama kawaida yao. Tunawashukuru sana kwa hilo.

Waheshimiwa Wajumbe waliopata fursa ya kuchangia kwa ujumla wao wapo 26 ambao kwa kweli si haba, Wajumbe 16 wamechangia kwa kusema moja kwa moja na Wajumbe kumi wamechangia kwa maandishi. Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba niwataje waliochangia moja kwa moja ni kama hawa wafuatao.

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
2. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
3. Mhe. Suleiman Sarahan Said
4. Mhe. Simai Mohammed Said
5. Mhe. Rashid Makame Shamsi
6. Mhe. Suleiman Makame Ali
7. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
8. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil
9. Mhe. Said Soud Said
10. Mhe. Panya Ali Abdalla
11. Mhe. Mohamed Said Mohammed
12. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali
13. Mhe. Shehe Hamad Mattar
14. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
15. Mhe. Hamza Hassan Juma
16. Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Waheshimiwa hawa wote nawashukuru wamechangia moja kwa moja michango yao tumeipokea maoni yao tumeyapokea, lakini vile vile katika yale maeneo ambayo yatahitaji kutolewa

ufafanuzi nitajitahidi kufanya hivyo, ili niweze kuwaridhisha Waheshimiwa Wajumbe na wale waliotia nia ya kuzuia vifungu waondoe nia hizo.

Waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao:

17. Mhe. Said Omar Said
18. Mhe. Juma Ali Khatib
19. Mhe. Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo.
20. Mhe. Waziri wa Ajira, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto
21. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale
22. Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
23. Mhe. Mgeni Hassan Juma
24. Mhe. Naibu Waziri wa Ajira, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto
25. Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda.
26. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma

Baada ya kuwashukuru wachangiaji wote hao sasa naomba kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya maeneo yaliyoguswa na Waheshimiwa Wajumbe kama ifuatavyo:

Kwanza nianze na ufafanuzi kwa Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) alitoa pongezi nyingi na tunazipokea pongezi hizo. Lakini pia alitaka *TRA* na *ZRB* iendelee kutoa taaluma kwa walipakodi nchini. Jambo la kulipa kodi ni jambo muhimu sana. Nichukue fursa hii kwanza kuwapongeza sana wananchi, wafanyabiashara na walipa kodi wote nchini ambao sasa wameelewa dhana kamili na umuhimu wa kulipa kodi kwa maendeleo ya nchi. Kwa kweli jitihada zetu kama Wizara ni kutoa taaluma na kuelimisha wananchi, lakini ile *compliance* yao ndio iliyochangiwa sana kukuza mapato ambayo hivi sasa tunayaona. Jitihada hiyo ningeomba sana iendelee na hasa kwa wananchi wengine waliokuwa bado hawajapata muamko wapate muamko kama waliopata wenziwao ili nchi yetu iweze kupiga hatua kubwa zaidi ya maendeleo.

Taaluma hiyo tutaendelea kuitoa kama inavyotoka sasa, inatoka kupitia semina, mikutano mbali mbali, vyombo vya habari, Televisheni na redio zote, vipeperushi, lakini pia huwa kuna michezo ya maigizo maalum nayo inaandaliwa kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kulipa kodi zao. Hili suala ni zuri ni suala ambalo litaendelezwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said, yeye alizungumzia suala la uondoshaji wa mali za umma. Hapa nizungumze tu kwamba kuna utaratibu mzuri tu ambao unafuatwa katika uondoshwaji wa mali za umma. Hivi sasa tayari tunayo sheria mpya Sheria Nam. 11 ya mwaka 2016 ambayo ndiyo Sheria inayotekelezwa na kanuni zake zipo katika hatua ya mwisho kabisa kukamilika. Vitu vyote vinavyonunuliwa na serikali ikiwemo magari, vyombo vyengine vya moto, *computer*, *photocopy* na majengo, huwekewa viwango vya kupungua kwa ile thamani yake kwa maana *depreciation*. *Depreciation cost* inawekwa na kuna viwango, *rate* maalum kwa ajili ya kupunguza samani ya vitu hivyo ambavyo huwekwa kwa *rate* hizo ndipo pia kunaweka utaratibu wa kujua kifaa kile au chombo kile kitumike kwa muda wa miaka mingapi.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hali hiyo inawezekana kukawa na chombo ambacho kinatakiwa kitumike kwa miaka minne na kwa kutumia fomula hii ya *depreciation* itafika miaka minne kwamba *book value* yake ikawa ni *zero,* lakini kile chombo bado kinaonekana kina uwezo wa kuendelea kutumika na serikali. Si busara kukiondoa maana kuna vyombo vyengine hata magari muda wao wa *book value* itasomeka kama *zero,* lakini bado kile chombo kinafaa kutumika, kwa hivyo si busara kukiondosha. Kuna utaratibu wa kufanya kinatiwa thamani tena upya *(revaluation)* halafu kinaendelea na mchakato ule ule wa kupunguza thamani yake hadi pale tutakapokiona kifaa kile sasa kimekuwa chakavu *(scrape)* ndio tunaweza tukakiondosha kwa taratibu zilizoelekezwa na sheria. Kwa hiyo hilo Mheshimiwa nikutoe wasi wasi suala hilo linafanyiwa kazi vizuri sana.

Lakini pia ulizungumzia suala la kuwa na *asset register* na ni suala ambalo nimeshalizungumza sana katika Baraza hili ni kwamba serikali kupitia mradi wa mageuzi au Programu ya Mageuzi ya usimamizi wa fedha za umma PFMRP ambayo inafadhiliwa na DFID, Norway pamoja na Denmark. Mradi huu upo na unafanyakazi Tanzania Bara na Zanzibar na tayari tumeanzisha daftari la mali za serikali na niliwahi kutoa taarifa kwamba Wizara tano tayari zimekwisha kukamilika utaratibu ule kule nyuma. Ndani ya mwaka unaokuja wa 2018/19 tunatarajia Wizara zote nyengine ziwe tayari zimeshawekewa daftari.

Daftari hili sasa litakuwa ni daftari la ki-*electronic* kwa hivyo takwimu zote zimekwisha kukusanywa, mali zote za serikali tayari zimeshatambuliwa na sasa zipo katika utaratibu wa kuingizwa na kila taasisi ya serikali itawekewa *computer* yake na kuweza kuziona *asset* zilizokuwemo katika taasisi ile. Utaratibu huwo unaandaliwa, tayari kama nilivyosema *asset* zimeshatambuliwa na nyengine tayari zimeshawekewa alama maalum (*beacon*) na kitu kitakachoendelea hivi sasa ni kuingizwa katika huwo mfumo ili daftari hili sasa liwe lipo *electronically* ambalo litaweza kuwa-*shared* katika taasisi zote za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hiyo Wizara yatari imeandaa sera ya usimamizi wa mali za serikali kwa maana *asset management policy* na sera hii sasa ipo katika rasimu na tunatarajia hivi karibuni itawasilishwa katika Kamati ya Uongozi ya Wizara kabla ya kupelekwa katika ngazi nyengine husika ili iweze kupitishwa kama ulivyoutaratibu.

Vile vile kama nilivyosema mwanzo kwamba tunakamilisha utayarishaji wa Kanuni za Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali ambayo ndani yake kutakuwepo na Kanuni inayoelekeza kuandaliwa kwa mpango wa uondoshaji wa mali za serikali yaani (*asset disposal plan)* na hii kama ilivyo kwa taasisi kulazimika kuwa na mpango wa ununuzi (*procurement*) lakini pia watatakiwa kwa mujibu wa kanuni hizi kuwa na mpango wa uondoshaji wa mali za serikali (*asset disposal plan*). Kwa hivyo haya yote yatakwenda sambamba katika kuimarisha usimamizi wa mali za serikali.

Mhe. Suleiman Sarahani ulizungumzia na hili umeshalizungumzia mara nyingi kuhusiana na hoja ya yule mtu mmoja ambaye hajalipwa fidia yake katika lile jengo ambalo eneo lile litajengwa jengo la Ofisi ya Bima Pemba. Kama nilivyowahi kusema kwamba tayari waliotakiwa kulipwa watu saba tayari wameshalipwa na hiyo ilikuwa kutokana na tathmini iliyofanyika kwamba hao saba ndio waliolekezwa walipwe. Lakini kama kuna mmoja kasahauliwa

nikuhakikishie mimi niko tayari tukae mimi na wewe lakini na uongozi wa Bima na ikibidi tunaweza kuja Pemba tukakaa na wahusika mbali mbali akiwemo na huo anayedaiwa kwamba bado hajalipwa ili kuweza kujua ukweli wa jambo hilo na kama anastahiki haki yake basi hatodhulumiwa na serikali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala jengine ambalo aliliuliza Mhe. Sarahani la kwamba kuna wazalendo ambao wanadhulumiwa haki zao na wawekezaji, kwa sababu kuna wawekezaji ambao wanawadhulumu watu haki zao. Lakini hili niseme tu kwamba sisi kama serikali tunasisitiza sana kwamba wananchi wanapo-*deal* na wawekezaji ni lazima wafuate taratibu za kisheria na kwamba lazima waingiane katika mikataba, ikiwa ameajiriwa basi lazima aingie katika mkataba na huyo muajiri wake. Lakini vile vile anatoa huduma basi ni lazima waingiane katika mikataba. Kufanya biashara hizi kiholela bila ya kuwa na mikataba madhubuti kwa mujibu wa utartibu utawaletea usumbufu sana, lakini pamoja na hayo serikali itaendelea kuhimiza na kufuatilia kuona kwamba wananchi wanapata haki zao. Lakini vile vile tunawafuatilia kuona kwamba wanaingia katika mikataba halali na wawekezaji wanaokuja nchini.

Pia ulizungumzia kwamba baadhi ya washiriki wa maendeleo hawana nia njema na ulisema kwamba wasituharibie bajeti zao kwamba bajeti zetu huwa tunaweka kwenye bajeti lakini fedha hizo hazitoki. Nikuhakikishie Mhe. Muwakilishi kwamba washirika wa maendeleo wote tunaowaingiza katika vitabu vyetu vya bajeti ni wale ambao tuna mashirikiano nao kwa dhati kabisa, wana nia njema na tunamashirikiano nao na kabla ya kuingizwa katika vitabu hivi huwa kushafanyika mazungumzo ya kutosha na mikataba imeshafungwa. Kwa hivyo hao sio wababaishaji. Suala la kuchelewa kupatikana kwa fedha hilo lina sababu nyengine mbali na hii na nimeshawahi kulitoalea ufafanuzi hapa, wakati mwengine huwa taratibu hazijakamilika. Lakini vile vile kuna masuala mengine ya ununuzi yenyewe kwa mujibu wa sheria zilizopo nchini na huwa yanachelewesha *displacement* ya fedha hizo.

Mhe. Mwenyekiti, jengo la Baraza la mji wa Chake Chake lililozinduliwa katika sherehe za Mapinduzi January 2018 kwamba linavuja kwamba jengo hili kweli lilizinduliwa katika kipindi hicho na lilijengwa kwa kupitia mradi wa huduma za mijini *ZUSP* na kwa kweli bado limo katika kipindi cha uangalizi ile *different powerability*. Kwa hivyo hio bado haijamalizika muda wake na lilitokea tatizo hilo dogo la kuvuja katika baadhi ya maeneo kwa sababu baadhi ya maeneo kwenye bati kulikuwa na tundu ambazo zilikuwa zinavujisha, hilo limeonekana na tayari mkandarasi ameshachukuwa hatua na ameshaziba tundu. Ningekuomba Mhe. Suleiman Sarahani ukatembelea tena utaona kwamba kazi imekamilika na bado kama litatokea tatizo kwa sababu muda wa uangalizi haujakamilika basi shughuli za marekebisho bado itakuwa ni jukumu la mkandasi tuliempa kazi hiyo.

Kuhusiana na suala la fidia za ujenzi wa barabara nao lina utaratibu wake lazima ifanyike thamani ikiwa nyumba ikiwa vipando na thamani ile ikeshafanyika ndio inayokuwa *base* ya malipo, Wizara ya Fedha tunakabidhiwa kupitia wizara husika. Kwa hivyo shughuli zote huko za kupitia thamani zinafanyika ama nyumba ama vipando na ikisharidhika kwamba hii sasa ndio orodha ndio inayoletwa na kufanyiwa malipo. Lakini suala la malipo mara nyingi sana huwa linaleta utata kwa baadhi ya watu kutoridhika, lakini wajue kwamba thamani hizo zinawekwa

kwa mujibu wa vigezo na sheria ambazo zinatawala nchi, wengine hawaridhiki ni jambo la kawaida ukimpa mtu kumi atataka ishirini, ukimpa ishirini atataka arubaini, lakini ni muhimu kuhakikisha kwamba tunazingatia vigezo, tunazingatia sheria na taratibu ambazo tumejiwekea wenyewe. Na kama kuna mtu anadhulumiwa na ikidhibiti hivyo, kaleta malalamiko yake basi suala la kuliangalia upya linafanyiwa kazi na ikionekana kwamba kuna haja huyo mtu kutizamwa upya madai yake yanaangaliwa bila kuathiri maisha ya wananchi au kuwatumbukiza wananchi katika hali ya umaskini.

Mhe. Mwenyekiti, malipo ya Viinua mgongo nilishawahi kulizungumza suala hili nilijibu hapa barazani katika Baraza hili katika kikao hichi hichi kinachoendelea na nikasema utaratibu wetu ni kwamba tunalipa katika makundi ya vipindi vya miezi mitatu mitatu. Siamini kwamba kuna watu wanazidi hapa na lazima tukiri kwamba kumetokea mafanikio makubwa katika ulipaji wa viinua mgongo ukiangalia hali halisi iliyopo huko nyuma. Huko nyuma hali ilikuwa sio ya kuridhisha sana na ilikuwa na sababu zake, lakini sasa tunajitahidi sana ndani ya kipindi cha miezi mitatu kama taarifa za mfanyakazi huyo zipo kamilifu hazina utata hazicheleweshwi kutoka taasisi yake na kupelekwa kwa ***CAG,*** ikishafanyiwa kazi malipo yanafanyika ndani ya kipindi cha miezi mitatu. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 nilisema hapa tumelipa jumla ya Shiling Bilioni 17.7 na tumewalipa wastaafu 1,057 hivi hawa wamelipwa, na bado tunaendelea kuwalipa wale wastaafu walioanzia kuanzia mwezi wa Januari kwa sababu hao mpaka mwezi wa Disemba, Januari hadi Mei ambayo maombi yao tayari tumeshayapokea katika Wizara ya Fedha. Kwa hivyo hakuna suala hilo la ubabaishaji serikali inafanya kazi kubwa sana na tuchukue kwamba serikali imebeba mzigo mkubwa zaidi kwa sababu mishahara imeongezeka, kwa hivyo na mafao yameongezeka, lakini pamoja na hayo yote serikali inachukua jukumu lake la kuhakikisha wananchi wanapata mafao yao kikamilifu.(*Makofi*)

Pia ulizungumzia suala la jengo la *Terminal II*, ukasema hili ni *Terminal II* au *Terminal III*, nilishawahi kuja kulisema hapa kwamba sasa rasmi serikali imeagiza jengo linalojengwa jipya litambulike kama ni *Terminal III* . Lakini ukataka kujua *Terminal I* ni ipi, ni ile uwanja ambao viongozi wetu wakuu wanautumia wakati wakisafiri na kuingia ile ni *Terminal I* kwa sababu ndio ilejengwa mwanzo lakini *Terminal II* ndio hii tunayoitumia sasa na jengo jipya ni *Terminal III.* (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ajira kwa vijana ulizungumza ni program muhimu na ukitizama hatujasoma bajeti ya serikali lakini tutakaposoma bajeti ya serikali tutalitolea maelezo ya kina kwamba ni eneo moja ambalo tumelipa kipaumbele sana katika bajeti ya mwaka 2018/2019, ajira kwa vijana kwa sababu tunaona kabisa hilo ni suala ambalo linahitaji kuwekewa mkazo na mazingatio maalum.

Lakini kwenye hilo tu niku-*brief* kwamba juhudi za serikali za kukuza uwekezaji hasa katika sekta ya uvuvi wa bahari kuu ni moja ya juhudi ya kukuza fursa za ajira, lakini pia kuanzishwa kwa viwanda, kutolewa taaluma ya ujasiriamali, lakini vile vile mikopo nafuu ambayo tunataka uendelezwe hasa kwa vijana ni katika juhudi za kuhakikisha tunatoa fursa zaidi za ajira kwa vijana wetu. Tuanzishe Banki ya Maendeleo, hili wazo umelitoa sio wazo baya kutegemeana na mazingira yaliyopo, kutegemeana na uwezo wetu, kutegemeana na soko. Suala lako linaweza likazingatiwa.

Lakini pia ulizungumzia suala la misongamano benki hili lishazungumzwa sana na wingi naomba nilitolee ufafanuzi kwa maana hapa nimeshalitolea ufafanuzi, kwamba hivi sasa benki yetu hii katika kutatua tatizo la msongamana inaweka mfumo mpya, kwa maana ya *Core Banking System* hiyo inakaribia kumalizika na tunatarajia ndani ya mwaka huu 2018 Inshaallah basi tutafikia mahala pazuri zaidi na tatizo hili linaweza kuondoka kabisa.(*Makofi*)

Lakini jengine benki hii inaongeza *ATM* lakini pia kuna huduma za *Internet bank* zinatolewa, huduma za M-*pesa, Ezy-pesa* zinatolewa, wananchi nazo hizi wazitumie, inawezekana taaluma benki inaendelea kutoa taaluma na naona kabisa kupitia *ZBC* taaluma hiyo pia inatolewa ya kutumia haya *ATM* na kutumia masuala ya *mobile services*. Haya yote yanafanyiwa kazi Inshaallah Mwenyezi Mungu akitujalia kwa lengo la kuondosha msongamano katika benki zetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Simai Mohammed Said, mwakilishi wa Jimbo la Tunguu alitaka kujua katika kila lita moja ya mafuta, fedha zinazoingia serikalini ni kiasi gani, na nitaomba nimtolee ufafanuzi kwamba kwa petroli, fedha zinazoingia serikalini katika kila lita moja ya mafuta ya petroli ni *excise duty* kwanza Shiling 80, *road license* shilingi 38, *infrastructure* (miundombinu) Shilingi 100, *petroleum levy* ni shilingi 350 na *road fund* Shiling 100. Kwa hivyo jumla ni Shilingi 668 lakini hiyo sasa jumlisha na ile *fee* ya *ZURA* ya Shilingi 100, kwa hiyo itakuwa ni Shilingi 768 kwa kila lita.

Na kwa upande wa *diesel, execise duty* ni shilingi 30, *road license* Shilingi 38, *infrastructure* ni Shilingi 100, *Petroleum levy* ni shilingi 350 na *road fund* ni Shilingi 100 na *ZURA fees ni* Shiling100. Kwa hivyo itakuwa ni 718, hivyo kwa kila lita moja ya *diesel* serikali inachukua shilingi 718 na kwa petroli Shilingi 768.

Mhe. Mwenyekiti, pia ulizungumzia suala hili la wafanyabiashara wanaponunua bidhaa kule Tanzania Bara wanalipa asilimia 18 *VAT* na wakija huku wanalipa tena asilimia 18, ni suala ambalo nimeshalizungumza mara nyingi na naomba niendelee kulitolea ufafanuzi kwamba ni suala linatokana na wenzetu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kubadilisha Sheria yao ya Fedha ya mwaka 2016, wamebadilisha na wana sheria yao na wana mamlaka yao, wamebadilisha na wakaweka vipo vigezo ambavyo mtu anayenunua bidhaa na kuisafirisha kuja Zanzibar inabidi avifuate ili aweze kunufaika na ile *zero rated* inayowekwa kule Tanzania Bara, na vigezo hivyo nimeshawahi kuvitolea maelezo katika Baraza hili na vina *condition* zake:-

1) Bidhaa hizo lazima ziwe zimetengenezwa kule Tanzania Bara
2) Ziwe zimenunuliwa moja kwa moja ama kiwandani ama kwa mtengenezaji wa bidhaa hiyo, lakini huyu mnunuzi naye pia awe *VAT registered,* lakini kuna hoja nyengine kwamba bidhaa hiyo lazima ihaulishwe itoke Bara iingie Zanzibar na itumike hapa sasa

Sasa hivyo ndio vigezo vya kuweza kupata *Zero rate* kwa upande wa Tanzania Bara kwa bidhaa inayokuja Zanzibar au inayohaulishwa kuja Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, sasa wengi wa wafanyabiashara wetu wadogo wadogo wanaokwenda kununua vitu Kariakoo hili linawapiga kwa sababu wanakosa sifa hizi, tukatoa rai ya kwamba waweze waruhusiwe au wahamasishwe kwenda kununua sehemu nyengine. Ninafikiri hilo liko wazi sisi tumeshalitoa maelezo sana

kwamba watu wako huru kwenda kununua popote wapo huru kwenda kununua Msumbiji, wapo huru kwenda kununua Mombasa, Kenya, Nairobi, *wherever* wako huru kabisa.

Lakini hii ni mujibu wa Sheria ya Fedha iliyowekwa na wenzetu mwaka 2016 na sisi tulijaribu kuzungumza athari zake, lakini bado inaendela kutumika. Kwa hivyo bado itabidi tuendelee kuheshimu sheria hizi na tufuate taratibu zilizopo. Lakini kuja kutoa ushauri kwa wafanyabishara basi na wao wajiunge pamoja wawe na nguvu za pamoja waweke *dealer* ambaye anaweza kwenda kununua vifaa au bidhaa hizo moja kwa moja kwa *supplier* ili waweze ku-*benefit* kutokana na utaratibu uliopo hivi sasa, ni lazima tubadilike kwa mujibu wa mazingira tulionayo kwa wakati huu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna hoja hii ya Mheshimiwa ulisema ya Mhe. Bakharesa kuwa *interest* ya kuwekeza bandari kwa upande wa Mombasa ni wazo zuri lakini ni suala ambalo litahusu muekezaji mwenyewe na *interest* yake, lakini pia litahusu pia na Serikali ya Kenya katika kutoa vibali vya uwekezaji hu. Sisi mkono wetu ulisema pale tumejaribu kushauri ni jambo zuri sisi tunalikubali lakini halimo ndani ya mmiliki ya Wizara ya Fedha au ya Tume ya Mipango kutoa ushawishi wa aina hizo.

Hoteli ya Bwawani haikufanywa vizuri tulizungumza hilo na hili limelitolea jibu juzi katika swali lililoulizwa na kwa mujibu wa kanuni zetu kwamba *Hansard* ipo, majibu yangu yanabaki kuwa yale yale kuhusiana na Hoteli ya Bwawani na ni sahihishe tu kwamba baadhi ya magazeti yaliandika kwamba tayari tumeshamnyan'ganya ile hoteli yule mwekezaji. Mhe. Mwenyekiti, taarifa sahihi hajanyang'anywa, tulimpa *notice* na kumtaka kwamba afanye haraka sana kuhakikisha kwamba anafanya kazi aliyotakiwa kuifanya kwa mujibu wa mkataba na nikatoa indhari kwamba asipofanya hivyo serikali haitosita kumchukuliwa hatua, hayo ndio maelezo niliyoyatoa lakini baadhi ya vyombo vya habari inawezekana kwa bahati mbaya sana waliripoti sivyo.

Pia ulizungumzia kuhusiana na kodi zinazotozwa Pemba hazitosaidia uwekezaji na lazima tuweke vivutio maalum. Ni kweli ni wazo zuri na serikali tayari imeanza ukitizama Sheria ambayo imepitishwa kwa *legal notice* ya uwekezaji mkakati imeweka mazingatio maalum kwa wale ambao watawekeza katika maeneo ambao tunayaona yako *less advantage.*Kuna mazingatio maalum, kuna vigezo maalum ambao vitafuatwa lakini niseme tu ndani ya mwaka 2018/2019, serikali inakusudia kufanya mapitio ya mfumo mzima wa kodi, kwa hivyo hayo mawazo yako tutayaangalia na tutayazingatia wakati ule utakapofika.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kuna swali jengine lilizungumzwa kuongezeka kwa deni la ndani, ni kweli deni limeongezeka lakini bado kuongezeka kwa deni hili lina afya kwetu, kwa sababu kama nchi ni lazima tukope na kwa sababu bado tunahitaji kuendelea kukopa ni lazima na tumeshawahi kuzungumzia kwamba ukopaji wetu sisi bado upo chini sana ni wa asilimia 15 ya pato la taifa, wakati watu wengine wanakwenda mpaka asilimia 45, asilimia 50 sasa itakuwa hatari lakini asilimia 15 bado tupo vizuri na tunaweza kukopa na tunaweza kukopesheka na deni letu linahimilika ambalo hilo ndilo nililozungumza, kwa hivyo tuko vizuri.
Lakini sababu ya kuongezeka deni hili ni kupatikana kwa fedha za mkopo wa jengo la *Terminal II* ndio lililo *push* ule mkopo lakini vile vile mkopo tuliokopa kutokana na *treasury bill*

hatifungani ya Shiling Bilioni 20 nayo imeongeza mikopo ya ndani. Kwa hivyo deni letu limeongezeka kutokana na mambo ya msingi ambayo tumeyafanya na sio kwamba tumekopa kiholela.

Mhe. Mwenyekiti, ulitaka tuweke *ATM* Dunga nafikiri pia na Mwera. PBZ wameshalisikia hilo na katika mazingatio ya maeneo mapya ya kuwekwa *ATM* basi Inshaallah kutokana na hali ya kibiashara katika maeneo hayo watakuwa na vigezo vyao watafuatilia na watakuja ku-*consult* pia wapate mawazo yako juu ya sehemu gani hasa unakusudia iwekwe, basi Inshaallah *ATM* hizo baada ya wao kuzingatia na vigezo vyao itafikiriwa kuwekwa katika maeneo hayo.(*Makofi*)

Mafunzo kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hasa katika masuala ya uhakiki mali, tunalichukua na kadri hali itakavyowezekana basi tutatoa mafunzo hayo kwa Waheshimiwa Wajumbe ili wajenge uelewa.(*Makofi*)

Lakini kuna suala la nguzo za umeme ziliopo *Victoria Garden* ulitaka hizi zisaidiwe jimbo lako, taasisi zinazohusika limesikia, ikiwa hii mali tayari haitakiwi kutumika katika serikali utaratibu upo wa kisheria kabisa wa kuondosha mali za serikali basi tu wewe peleka maombi yako kwa taasisi inayohusika ili taratibu ziweze kufanyika.

Mhe. Rashid Makame Shamsi alizungumzia suala la kitabu chetu *numbering* kidogo zina matatizo nikubaliane naye, kuna mahali kweli kuna namba zimeruka na hili lilitokana na *setting* wakati kitabu hichi kinachapishwa kule *gorvenment printing press*. Sisi tumeyaona makosa na namshukuru sana na yeye pia kwa kuyaona, lakini pia hayaathiri yale maelezo ya ndani ya kitabu ni *numbering* tu ya *paragraph* katika hasa kurasa za mwanzo za kitabu changu.

Mhe. Mwenyekiti, pongezi tumezipokea alitaka kuona kwamba tunafanya mapitio ya kuangalia uwezo wa vianzio vya mapato ili tuweze kulinganisha na malengo tunayoyaweka, hilo nimeshalitolea ufafanuzi litafanyiwa kazi katika mapitio ya mfumo mzima wa kodi.

Taaluma kwa walipa kodi nimeshaizungumza *Asset Register* tayari nimeshaizungumza lakini pia alitaka tuandae Sera ya Kodi na Usimamizi wa Uchumi ni wazo ambalo tunalichukua.

Pia Mhe. Shamsi alitaka kujua je, tuna uwezi wa kufikia malengo tuliyojiwekea ya uchumi wa kati tukifika 2020. Kwanza nikwambie tu Mhe. Shamsi bado liko pengo la kufikia ya malengo ya mwaka 2020 na ili tuweze kufikia malengo ya 2020 ni wajibu kwa wananchi wote tufanye kazi kikamilifu, ukiacha watoto wa chini ya umri wa miaka kumi na tano na wazee wanaozidi miaka sitini na tano. Sasa hii *work force,* umri wa watenda kazi lazima tunahakikishe tuna tenda kazi kweli kweli, tunaondoka na ufisadi wa kila aina tukiweza kufanya hayo uchumi wetu utakua kwa haraka zaidi na malengo tuliyoyaweka tunaweza kuyafikia. Lakini hata kama hatutoyafikia bado tuna utaratibu wa kwamba mipango mizuri tuliyoiandaa katika *vision 2020* tunataichukua katika kuandaa dira mpya ya maendeleo katika nchi hii ambayo mchakato wake tayari umeshaanza.

Mhe. Mwenyekiti, misingi ya maji ya mvua ulizungumza pia Mheshimiwa. Niseme tu ujenzi wa msingi wa maji ya mvua katika eneo la Meya tayari umekamilika na kuunganishwa na mtaro mkuu wa *system E na* tatizo la kutuama kwa maji eneo la Meya limemalizika hivi sasa. Lakini

pia ujenzi wa msingi katika eneo Magomeni hadi barabara ya Mpendae nayo umekamilika. Hata hivyo msingi huu bado haujaunganishwa na mtaro mkuu wa Jang'ombe kazi ambayo inafanyika hivi sasa. Ninafikiri zipo karibu kama mita 366 za kuunganishwa ili nao mtaro huo uweze kufanya kazi vizuri.

Lakini pia kuna *system C* ambayo tayari umeanza na utajumuisha ujenzi wa msingi wa maji ya mvua maeneo ya Mwantenga, Nyerere, Amani. Mfumo huu ukikamilika utaondoa tatizo la maji ya mvua maeneo ya Magogoni, eneo la Nyerere, Bwawa la Mwantenga na Bwawa la Sebleni. Aidha mfumo huu ukikamilika utapunguza maji kwa kiasi kikubwa eneo la Mwanakwerekwe.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuyazungumza hayo Mhe. Suleiman Makame Ali yeye alitoa indhari ya kusema kwamba ataweka buti, lakini alizungumzia suala la viinua mgongo kwa wastaafu hili nimeshalieleza lakini pia alizungumza suala wa uwekaji wa taa hasa sehemu za Chake Chake. Lakini nimwambie tu kwamba mradi wa *ZUSP* awamu ya pili umezingatia hilo na taa zitawekwa katika miji yote mitatu ya Pemba. Mji wa Wete, Chake Chake na Mkoani na hivi sasa hivi wakandarasi wanafanya kazi ya ubunifu kwa maana ya *design* kwa ajili ya uwekaji wa taa hizo.(*Makofi*)

Kwa hivyo Mheshimiwa buti yako ondoa hilo suala linafanyiwa kazi lakini vile vile Mfuko wa Barabara huu nilisema katika majibu yangu hapa wakati najibu suala moja kwamba tutakaa Wizara inayohusika, Wizara ya Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ tutakaa na wenzetu wa *Road Fund*, tunatakaa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ili kuona jinsi gani sasa tunazitumia fedha za Mfuko wa Barabara katika kuimarisha barabara za ndani na hili pia nataka kulisema kuliunganisha na lile alilozungumza Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) kwamba kazi hiyo tutaifanya *immediately* baada ya kumalizika kwa kikao hiki cha bajeti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub alizungumzia kadhia hii ya Benki ya *FBME* na hii inawagusa wengi, inawagusa wananchi wengi na hata humu Barazani wapo wanaoguswa na kadhia hii lakini kama ulivyo utaratibu wa kisheria na kwanza niseme benki hii imefutiwa leseni. Ninafikiri hali ya sasa ni bora zaidi kuliko pale ambapo benki hii ingeli-*operate* kwa sababu isingiweza ku-*operate* leseni yake imefungwa na isingeweza kufanya kazi na benki nyengine yoyote dunia. Sasa hilo lazima tulikubali ndio mambo haya yanapotokezea lazima tukubaliane na *situation* hiyo. Lakini kiutaratibu baada tu ya kutokea hili suala kwa benki yoyote ile, Bima ya Amana ndio inayochukua sasa dhamana, kwa maana ya *Deposited Insurance Board* ambayo hiyo imekaa na tayari imeshalipa kwa mujibu wa taratibu kila mteja wa benki ile lakini *regardless* na *amount* ambayo wameweka wameshalipa milioni moja na laki tano na sasa kazi inayoendelea kufanyika ni kuangalia sasa mali za benki lakini na kuhakiki madeni yote ya wateja na baadae hatua zitafuata kwa mujibu wa hali itakavyokuwa baada ya kuainisha madeni yaliopo, lakini vile vile kuainishwa na *assets* au amana zilizokuwepo au mali zilizokuwepo za benki hiyo na kuona ndugu zetu hawa waliokuwa na akaunti zao pale watafidiwa kwa kiasi gani kwa mujibu wa taratibu zao.

Suala hili lipo lifanyiwa kazi na Benki Kuu. Kwa hivyo ningewaomba tu wawe wastahamilivu waangalie sheria na taratibu zinavyochukuliwa. Alizungumzia suala la haki na sheria lakini pia kwa upande wa haki wangepaswa walipwe zote, hiyo ni haki lakini vile vile tuangalie upande wa sheria, sheria zinaelekeza jinsi ya kulishughulikia suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ununuzi wa umeme suala hili tumelizungumza mara nyingi na lina kamati kupitia kamati ya vikao vyetu vya SMT na SMZ vinafanyiwa kazi hasa katika suala zima la deni la umeme ambalo sisi *ZECO* shirika letu la *ZECO* linadaiwa na *TANESCO* lakini vile vile na miundo mbinu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafidiwaje katika suala hili tuliache kwa sababu bado linaendelea kufanyiwa kazi na *ZRB* wenzetu wanafanya kazi kwa mujibu wa sheria kwa hivyo tunaomba tu tuwape mashirikiano wanapofanya kazi hizo za kukamata wale wahalifu tuwape ushirikiano mzuri na kubwa zaidi tuzidi kuelemishana na kuwaelimisha wananchi wetu wakubali kufuata sheria ya kulipa kodi kwa hiari na bila ya kushurutishwa.

Sheria ya kwamba kuna kikomo cha wafanya biashara kusafiri nacho cha $10,000 Mhe. Jaku alisema hiki kinadhorotesha biashara lakini niseme tu kwamba hii sheria ya kutoruhusika mtu kusafiri na kiwango zaidi ya $10,000 si kwa Zanzibar wala Tanzania peke yake ni dunia nzima na sisi tumezowea kama wafanya biashara kutembea na ma-*cash*, sasa hali hiyo duniani imeshabadilika wewe ukienda na *cash* sasa hivi ukianza kulipa kwa ma-*cash* watu wanakushangaa huko duniani kwa hiyo sisi tunashauri kwa sababu si suala la Zanzibar wala Tanzania peke yake ni suala la kidunia hata hizo nchi nyengine tunaposafiri ukionekana umekwenda na kiasi kinachozidi $10,000 utahojiwa nazo, lazima uwe na taratibu cha kuchukua kima kikubwa hicho cha fedha sisi tungewashauri wafanya biashara wetu wakatumia mifumo ya kibenki ambayo iko wazi na haina usumbufu lakini pale wanapotaka sasa kwenda kiwango kikubwa zaidi basi wajaze fomu zile za ku-*declare* kiwango ambacho watataka kusafiri nacho.Wala halina utata ajaze fomu tu na hii ipo kwa mujibu wa sheria nambari 10 ya mwaka 2009 na udhibiti wa fedha haramu kwa hii ipo kwa mujibu wa sheria na kanuni zake ni kanuni nambari 70 ya mwaka 2015 ni sheria ambazo tumezipitisha na muhimu kuwahimiza wananchi kuzifuata sheria hizo.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil namshukuru kwa pongezi zake alizotoa namshukuru pia Mhe. Panya naye alizungumzia suala la takwimu Mhe. Panya Abdalla Ali ni kweli takwimu ni kitu muhimu kwa sababu ndizo zinazoturahisishia katika upangaji wa mipango yetu ya maendeleo lakini vile vile na kufanya tathmini.

Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) alikuwa na mengi kidogo na alikuwa wakati wa hatua za mwisho mwisho atanistahamilia kama mengine yameweza kuya-*capture* kwa sababu na yeye *speed* alokuwa nasoma alikuwa anakwenda kwa *speed* kubwa, lakini nitajaribu yake ambayo nitaweza kuyatolea ufafanuzi ni kwamba moja alizungumzia suala la Mfuko Mkuu wa Serikali. Mfuko Mkuu wa Serikali una matumizi mengi na alitaka kujua yale matumizi mengineyo na hii ni kwa nchi zote si Zanzibar kwamba lazima kuwe katika Mfuko Mkuu wa Serikali matumizi mengineyo pale tunapopata maafa na majanga fedha hizi ndizo zinazotumika, kuna mambo ya dharura yakitokea lazima yatumike kupitia mfuko huu lakini safari za Waheshimiwa Viongozi wetu waliopo madarakani na wastaafu na malipo yao kwa mujibu wa sheria zinatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa hayo nido matumizi mengineyo ambayo yamo ndani ya Mfuko

Mkuu wa Seikali nafikiri kabisa mheshimiwa atatuamini na hili suala linafanyiwa kazi pale tunapopata dharura basi hatuna pa kukimbilia isipokuwa Mfuko Mkuu wa Serikali.

Lakini hata mara hii mabadiliko ya mishahara ilipotokea na malipo kwa ajili ya viinua mgongo yalipoongeza tusingekuwa na vifungu lakini tulikimbilia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, haya ni matumizi ambayo yanatumika na nadhamini Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) ataridhika na kuliachia fungu hili lindelee ili tuweze kufanya kazi kama tulivyokuwa tukifanya kazi huko nyuma.

Tume ya Mipango alizungumzia ni miradi mingapi toke kupitishwa kwa Sheria ya *PPP* kwanza niseme kwamba sheria ya *PPP* ilivyotungwa tulipata uzoefu wa nchi nyingi ni sheria moja ngumu sana na nchi nyingi ambazo zilianza na utaratibu wa *PPP* huko mwanzo zilifanya makosa na sisi tumepata bahati ya kunufaika na *experience* yao makosa yao sisi walitupa nafasi ya kujifunza kwa hiyo sisi tulijifunza kwao na tukaja na sheria hii, kwa hiyo sheria imefanyiwa kazi kwa umakini mkubwa na niseme tu tuokea kupitishwa kwa sheria ile kuna miradi kumi na moja ya *PPP* ambayo imeainishwa na miradi hii iko katika hatua mbali mbali ya kufanyiwa maandalizi.

Hilo ni suala la *PPP* lakini pia kuna suala la miradi ya *ZIPA* Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) alitaka kujua ni miradi mingapi ya *ZIPA* ambayo iliyoombwa, miradi mingapi iliyopitishwa na miradi mingapi iliyokwama. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 miradi iliyoombwa maombi yaliyopokelewa ya miradi yalikuwa ni miradi hamsini na sita na miradi iliyopita ilikuwa ni miradi thelathini na nane na miradi iliyokwama ni miradi kumi na nane na hiyo miradi iliyokwama kuna miradi ambayo haikukidhi viwango, miradi sita haikukidhi viwango lakini pia miradi saba haijathibitishwa baadhi ya sheria, baadhi ya matakwa ya sheria kwa mfano *Shareholders* hawajaainishwa vizuri zile *Policy Registration Certificate* hazijatolewa na hawajaonesha kama kweli wana fedha *proof of fund* bado hazipo kwa hiyo miradi hiyo imekwama na miradi mitano bado haijarudishwa baada ya kuleta maombi yao kwa hiyo hizo ndio takwimu kwa ajili ya miradi inayopitia kupitia *ZIPA.*

Lakini vile vile alitaka kujua malengo yetu kimiradi kila mwaka kuna malengo ya kupitisha miradi hamsini na kifedha tumeweka *target* ya kwamba basi angalau kwa kila mwaka tuwe na miradi yenye thamani ya US$ 90,000,000 hilo ndio lengo ambalo lipo wakati wengine tunalifikia, wakati mwengine tunalipindukia, wakati mwengine hatulifikii lakini hayo ndio malengo na kwa mwaka 2018/2019 bado lengo letu liko hapo na tutafanya jitihada kubwa zaidi ili kuhakikisha kwamba malengo hayo tunayoyaweka yanafikiwa kila mwaka na hivi karibuni tu wenzetu wa *ZIPA* wametoa muongozo mpya kwa wawekezaji na muongozo huo tayari unasambazwa na kutolewa kwa wawekezaji mbali mbali ambao wameonyesha nia ya kutaka kuekeza katika nchi.

Kuna suala hili la mashirika yasioleta ripoti Barazani na hapa naomba niseme kwamba hivi karibuni tumefanya mapitio Sheria yetu ya Mitaji ya Umma sheria nambari 4 ya mwaka 2002 kifungu cha 27 kimefanyiwa marekebisho na kutaka kwamba ripoti sasa za mashirika lazima kwanza zijadiliwe katika Baraza la Mapinduzi na baada ya kujadiliwa katika Baraza la Mapinduzi na kupata baraka za Baraza zitawasilishwa katika Baraza la Wawakilishi hilo

tumeshalitolea ufafanuzi ningelimuomba Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) akastahamili ndani ya mwaka huu Insha'Allah taarifa hizo tutaanza kuzileta baada ya kupitisha bajeti hii.

PBZ riba imepungua amepongeza na nashukuru lakini pia alizungumzia kwamba ni vyema basi kuiga mfano wa *NMB* wa kukopesha wafanya biashara wadogo wadogo halafu *PBZ* iige mfano huo ni wazo tumelichukua lakini kila ina taratibu zake, kila benki ina *process* zake, kila benki ina *policy* yake hili ni wazo zuri wenzetu wa PBZ wamelisikia na wako tayari kuongeza wigo wa kupata wateja wengi zaidi na wakiona kwamba suala hili nalo lishakuwa tayari na lina manufaa kwao basi ni suala ambalo linaweza likachukuliwa.

Suala la Mfuko wa Barabara na *Feeder Road* hili limeshalitolea maelezo lakini pia mheshimiwa alitaka kujua kiashiria kimoja nafikiri ilikuwa ukurasa wa S 015 wa kile kitabu kuna sehemu pale kuna *gape* 000 nikiri kwamba pale palitokea na *typing error* nitarudi kuangalia *exactly* ni viashiria gani vilipaswa kuwepo pale lakini wakati mwengine wakati wa uchapishaji wa hivi vitabu na huwa vinafanywa kwa nyakati ambazo sio rafiki kwetu kuna mambo mengine huwa yanaruka ruka kwa hiyo pale palitokea tatizo hilo la kukiukwa namba zilizokuwepo pale.

Lakini kuna sehemu nyengine ulizungumza za ufuatiliaji wa raslimali za nje ukataka kujua ni kiashiria gani ukitizama pale chini mstari kipo kiashiria lakini kimeruka kutoka kwenye *line* yake kimekuja nyuma ukisoma tu utaiona kwamba ile 888 ni idadi ya mikutano na washirika wa maendeleo itakayofanyika ndio kiashiria chenyewe, ndiyo hayo mambo ninayoyasema wakati wa uchapaji kuwa kuna vitu kidogo vinakuwa *misplace* na vyengine vinakuwa *omitted* kwa makosa ya kibinadamu, lakini tunakushukuru sana kwa *observation* yako na Insha'Allah tutakuwa makini zaidi kuhakikisha lakini hasa tuwe na muda mzuri wa kutayarisha wa kutayarisha vitabu hivi ili watendaji waweze kuvi-*cross check* kabla kuwasilisha katika Baraza hili.

ATM nasema *ATM* nyengine hasa za Mwanakwerekwe zimeshapitwa na wakati *PBZ* Mhe. Mwenyekiti imeleta *ATM* mpya zipo mpya ambazo zinaendana na mifumo ya sasa ya kidunia kwa hiyo hizi zinazowekwa sasa hivi zote ni *ATM* mpya na zinakwenda na mifumo inayokubalika kwa hiyo kama kuna moja ambayo anaitilia mashaka basi *PBZ* haitasita ikiwa ina kasoro za kiutendaji sasa haitosita kufanya mabadiliko ya ATM hiyo.

Pongezi kwa mfuko wa *ZSSF* na Bima tunazipokea pongezi hizo Mhe. Mohammedraza tunakushukuru sana kwa mchango wako, Mhe. Shehe Hamad Mattar jengo la Wizara ya Fedha Pemba kumetokea nini hili tushalitoa maelezo sana na kwamba huyu mkandarasi ni raia wa Kenya tunajaribu kuchukua hatua mbali mbali za kumtafuta hana mali inayoweza kukamatwa hapa kwa hivyo hatuna cha kushika angalau angekuwa na mali tungeweza kesi iko mahakamani na bado mahakama inaendelea kumtafuta kokote uko aliko na akipatikana basi ataletwa katika vyombo vya sheria, lakini hatuna jibu zaidi ya hilo kwamba huyu mtu bado yuko nje ya nchi hapa hana *asset* suala liko mahakamani na anafuatiliwa kwa taratibu za kimahakama akipatikana basi atafikishwa katika mkono wa sheria ili hatua za kisheria ziweze kuchukua mkondo wake.

Lakini nhili jengo la Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto Mwanakwerekwe nadhani jengo ujenzi unaendelea katika ile ghorofa ya pili linaendelea vizuri wenyewe wapo

wanajua hivyo na tunatarajia kwamba ujenzi ule utakamika ndani ifikapo mwezi wa Disemba mwaka 2018, fedha kwa ajili ya ujenzi ule zipo kamili wala hazina matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Fumba alilozungumzia Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame na la utanuzi wa barabara ni masuala tunayachukua, tunayapokea tutakaa naye, tutakaa na wenzetu wanaohusika na vyombo hivi mbali mbali ili kuweza kuona tunayachukuwaje maoni ya Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame.

Mhe. Hamza Hassan Juma Mfuko wa Barabara ushauri nimeshasema kwamba tutakaa, alizungumzia suala la urasimu. Sisi wakati mwengine si suala la urasimu lakini suala la taratibu za kisheria za manunuzi na hili niliwahi kulitolea ufafanuzi, kwamba sheria yetu wakati mwengine inaweza ikachukua muda ili kuhakikisha tunachokipata kwamba kipo kwa mujibu wa sheria tulizozitunga sisi wenyewe. Lakini tutakaa pamoja taasisi zote zile nilizozitaja, taasisi tatu na tutaona jinsi gani ikiwezekana kubadilisha *formula* ili fedha zaidi zipatikane kwa Serikali za Mitaa kwa ajili ya ujenzi wa barabara za ndani. Hilo ni wazo ambalo sisi tunalichukua na tutalifanyia kazi.

Vifaa vya UUB tayari mchakato wa ununuzi umeshaanza, mtambo wa lami, *paver* pamoja na *sprayer*. Lakini pia nimwambie tu kwamba faida kwa wakopaji wafanye utaratibu wa kuonana na viongozi wa *PBZ* kwa sababu yeye ni mkopaji mkubwa ikiwa taasisi, ikiwa mtu binafsi tunaweza tu kwenda kuonana nao wakawa pengine na mazingatio maalum juu ya *rate*.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuhusiana na kodi kwa wale wanaolipwa madeni yao, kodi ipo kwa mujibu wa sheria na tutaomba tu kwamba wale wote wanaostahiki kulipa kodi walipe kodi zao, hazina mjadala kwenye hilo. Masuala ya makubaliano na tutaomba tu zile taasisi zisiweke madeni ya wateja au watoa huduma katika taasisi. Hilo tutalisimamia kwa ukamilifu, lakini suala la kodi bado tubaki kuwa vile vile.

Benki ya *PBZ* inafanya utaratibu wa kuanzisha *Visa Card* na *Master Card*.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa majumuisho yako ya ufasaha. Mhe. Jaku Hashim Ayoub nimekuona kuhusu utaratibu lakini nakuomba ukae. Sikuruhusu sasa hivi kuhusu utaratibu Mhe. Jaku.

Mhe. Waziri nakushukuru sana kwa majibu yako nakudhihirisha hayo kuwa umetoa ufafanuzi, kuna waheshimiwa wawili ambao waliweka nia ya kuzuia mafungu nao wamejitoa wamesema wameridhika na majibu. Wameniletea hapa ni Mhe. Simai Mohamed Said pamoja na Mhe. Suleiman Makame Ali.

Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa sasa naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja hiyo, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja imetolewa iamuliwe)

(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU F01 – WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Kifungu F0102	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	27,557,593,000

Mhe. Mwenyekiti: Watendaji wa wizara mnaweza kushuka chini mkamsaidia waziri.

Kifungu F0103	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	68,756,246,000
Kifungu F0104	Idara ya Fedha za Nje	467,602,500,000
Kifungu F111	Bodi ya Mapato Zanzibar	405,876,307,000
Kifungu F0112	Idara ya Forodha *TRA*	166,097,306,000
Kifungu F0113	Idara ya Kodi za Ndani *TRA*	135,378,573,000
Kifungu F0114	Idara ya Mitaji ya Umma	6,713,577,000
	Jumla Kuu ya fungu F01	**1,277,982,102,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU F01 - WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Kifungu PF0101

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru hoja yangu ni kuhusu Benki ya *FBME* pesa zimekaa muda mrefu na tumeambiwa pesa hizi ziko salama na wananchi wana pesa zao wakiwemo wawakilishi na wananchi wa nje, na hizi pesa ziko Zanzibar na benki iko Zanzibar na sheria wanayotumia ni ya Zanzibar. Nilikuwa nataka ufafanuzi wa Mhe. Waziri pesa zimekaa muda mrefu na vile vile hata Mwanasheria Mkuu akinyanyuka si vibaya akatueleza hiyo kesi Marekani imehukumiwa vipi kuhusu pesa zile.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub hukutia nia na katika orodha ya waliotaka kuzuia mafungu wewe jina lako halimo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa mimi sikubahatisha hata *hansard* ukienda kuziangalia zipo, nilisema suala hilo na siwezi kuinuka tu nikakurupuka mimi usingizini, *hansard* ipo na niko tayari kuwajibika.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub nakufahamu sana *hansard* zipo lakini zipo inawezekana ni *hansard* ya kuwa umechangia lakini hukutia nia kama utazuia fungu hili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi sikurupuki nilisema nazuia fungu na tuangalie *hansard* kama utaniruhusu nikachukue dakika moja, siwezi kukurupuka tu naomba busara za kiti chako zitumike, mimi sikurupuki tu ninavyokwambia nilisema na kitu kiko wazi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kwa vile umesema kiti changu naomba busara itumike basi na mimi natumia busara hiyo ya kumwita Mhe. Waziri akupatie ufafanuzi wa hayo uliyochangia.
Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na hili tayari nimeshalitolea ufafanuzi Mhe. Jaku Hashim Ayoub pengine hakuridhika na ufafanuzi nilioutoa. Lakini unabaki vile vile kwamba sheria zinazotawala *Bank* za *Financial Institution* ni Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzani kwa maana ya Sheria ya *Banking and Financial Institution Act* (*BAFIA*) ya 2006, hiyo ndio sheria. Kwa hiyo sio sheria za Zanzibar na haya mambo yote yanayofanyika benki ikifutiwa usajili wake au ikifilisika basi utaratibu unaotumika kwa Benki ya *FBME* ndio utaratibu huo huo utakaotumika kwa benki zote.

Mhe. Mwenyekiti, na nimeshasema kwamba kuna Bima ya Amana (*Deposit Insurance Board*) ambayo imeshakaa na wateja wote wameshalipwa 1.5 milioni na taratibu nyengine za ku-*assess* mali za benki hii pamoja na madeni ya benki hii zinafanywa chini ya usimamizi wa Benki Kuu. Kwa hiyo, hayo ndio majibu na popote atapokwenda atapata majibu hayo hayo hakutakuwa na majibu mengine, Mheshimiwa namuomba tu akubaliane tuendelee kwa sababu utaratibu unaendelea wa kisheria.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake lakini ningemuomba Mwanasheria Mkuu akainuka tu akatueleza ile hukumu iliyotoka Marekani haikufilisiwa ile benki zile pesa ziko salama.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub nimekufahamu lakini Mhe. Waziri tayari ameshakujibu hakuna haja ya kutaka Mwanasheria Mkuu aweze kusema tena na nadhani itakuwa jawabu ndio hiyo hiyo. Kwa hiyo, Mhe. Jaku naomba tuendelee.

Kifungu PF0101	Programu Kuu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma	57,858,640,000
Kifungu PF0102	Programu Kuu ya Usimamizi	

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilieleza kusikitishwa sana na jinsi Baraza lako tukufu linavyodharauliwa wakati limeshatoa maazimio ya kuleta ripoti hii Barazani, sasa hivi kweli tulibadilisha ripoti kuipeleka BLM. Lakini inasema sheria *Annual Report* sijui kama Kizungu sijui au nasema Kidonge maana yake kila mwaka iletwe sheria hii hapa Barazani, lakini bado sheria hii haijawahi kuletwa kama taasisi nyengine. Taasisi ambazo zililetwa ni *ZAECA* pamoja na Taasisi ya *ZAWA*.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, ripoti tayari kama ni ripoti hizi anazozungumza za *Annual Report*, Ripoti ya *CAG* itawasilishwa kesho na tayari Waheshimiwa Wajumbe wote wameshapatiwa na ripoti hii inaingiza pia Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kitabu hiki hapa. Kwa hiyo, taarifa yote itakuwemo humu na sisi kama mawizara utakapofika mwezi wa Septemba tutatoa maelezo juu ya yaliyoonekana na *CAG*. Kwa hiyo, taarifa hizo zinajadiliwa na tutapata fursa ya kujadiliwa ndani ya Baraza hili. Nadhani lugha yake na ya kwangu tunafahamiana ya Kidonge, kwa hivyo nadhani atanifahamu juu ya hili mheshimiwa.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nadhani hatwendi sambamba na Mhe. Waziri kuna sheria ambazo inataka Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali kuleta ripoti zake hapa Barazani, na hapa nimekwenda kwenye *specific ZIPA*. *ZIPA* ni taasisi moja ambayo inatakiwa kuleta Mhe. Waziri yeye amenambia ya *CAG*, yeye *CAG* mwenyewe anataka kuletwa kwa sababu maiti anakoshwa lakini na yeye aoshwe yule mtu akifa. *CAG* mwenyewe anataka kuletwa hapa na haleti lakini hata hii *ZIPA* mimi nimekwenda specific kwenye sheria ya *ZIPA* hailetwi hapa inataka kuleta. Mheshimiwa hapa nataka nilizuie fungu hili mimi niondoke nalo kwa sababu wamedharau Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa, kama alivyosema kwanza kuna aina mbili za uwasilishaji wa ripoti. Kuna ile ambayo ameisema Mhe. Mohamed Said Mohamed ambayo amessoma sheria ya *ZIPA*. Lakini Mhe. Waziri amemjibu kama ukisoma Sheria ya *ZIPA* umesome pia Sheria ya Mitaji ya Umma ambayo ndio inayosimamia na kuongoza mashirika na taasisi zote hizi zinazojitegemea za serikali.

Kwanza *CAG* nae kila mwaka huleta ripoti yake ambayo pia huingiza ripoti ya mashirika, lakini kwenye ile *specific* ambayo anaitaka Mhe. Mohamed Said Mohamed ambayo anasema ripoti ya kila taasisi inatakiwa iletwe iwe na mambo matatu.

(i) *Statement of Cooperate Strategic*
(ii) *Annual Report*
(iii) *Auditors Report*

Utaratibu wake umebadilishwa sasa hivi, zamani ilikuwa kila waziri anatakiwa alete ile ripoti baada ya kupata kwa *CAG* aiwasilishe moja kwa moja Barazani. Sasa hivi utaratibu wa kisheria ni kwamba lazima kwanza ipelekwe Baraza la Mapinduzi na baadae Baraza la Mapinduzi ndio inatoa idhini ya ripoti zile kuja Baraza la Wawakilishi.

Sasa hoja ya kisheria ni hiyo na hatutoweza kupinda sheria itabidi tuifuate, atusubiri kwanza tuende Baraza la Mapinduzi tukishatoka Baraza la Mapinduzi hizo sheria zote na taarifa kama zilivyotajwa kwenye Sheria ya Mitaji ya Umma na sheria nyengine *specific* ya kila taasisi ambayo imeeleza utafratibu wa kuleta sheria Barazani utaletwa kwa utaratibu wa kufuata sheria ulioelezwa kwenye sheria ya Mitaji ya Umma kwenye kifungu cha 27. Nashukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwanasheria Mkuu. Mhe. Mohamed Said Mohamed.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, sikufikiria kabisa kama Mwanasheria Mkuu, Mwanasheria msomi anaweza kuzungumza jambo lisilo na msingi wala sheria isiyo na mashiko katika Baraza hili.

Hapa tunakwenda *specific* na ripoti hii *Annual Report* ndio inavyozungumza mwanzo. Sasa tangu hiyo BLM inakaa mara ngapi kwa mwezi. Mimi nataka nilichukuwe hili fungu haiwezekani BLM ina vikao vyake vingi inakaa haijapelekwa mpaka leo au wanadharau Baraza lako tukufu na maazimio ambayo tumepitisha hapa wakati pia Makamu wa Pili wa Rais ndiye Kiongozi wa Serikali kwenye Baraza hili nae kainua mkono yule pale pia wanadharauliana wenyewe kwa wenyewe tunakuwa na mzungumko. Siwezi kusubiri kwa hili mimi nataka niiondoe sheria hiyo, nilichukuwe fungu hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mohamed Said Mohamed nadhani serikali imejibu na unasema kuwa Baraza letu linadharauliwa, lakini nahisi katika majibu ya Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu wamesema tayari ipo katika taratibu baada ya kutoka Baraza la Mapinduzi basi italetwa kwenye Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, nakuomba tu Mhe. Mohamed Said Mohamed ukubaliane na hoja zao kuwa wataleta na *hansard* zitaeka sawa kuwa wamekusudia kuzileta na wamesema zitaletwa hizo ripoti. Naomba Mheshimiwa ukubaliane na hilo.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme tu umekuwa "mserikali" unaanza kuwajibiya na hupaswi kuwajibia wajibu wenyewe. Mheshimiwa umetoa muongozo na mimi naheshimu sana kiti chako, lakini kama unasema hivyo basi tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mohamed Said Mohamed kiti sio mserikali Mheshimiwa nafata taratibu na zile kanuni tunazozitumia na kauli ya serikali na majawabu wametoa ndio niliyokuelekeza Mheshimiwa. Kwa hiyo siwi mserikali ila nitakuwa ni mtendaji ndani ya Baraza la Wawakilishi. Nakushukuru kwa vile umenikubalia mheshimiwa. (*Makofi*)

Kifungu PF0102	Programu Kuu wa Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma	19,919,537,000

Kifungu PF0104

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti, kwa nia safi kabisa nilipokuwa nikichangia inawezekana Mhe. Waziri yeye amesahau, ndio naona nipate fursa ya kumkumbusha. Wananchi wamenituma kamba wanadai Mabaraza ya Miji matatu ya Wete, Chake Chake na Mkoani kuna malimbikizo ya mshahara hadi leo. Sasa nilimuuliza katika kuchangia kwangu hapa je, katika hili deni la ndani nalo limo la Mabaraza. Shilingi 123,144,000 hajazitolea maelezo naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo ya ziada, sikulisema kwamba sikutoa ufafanuzi nimetoa ufafanuzi katika masuala yote, lakini suala la malimbikizo ya mishahara hilo ni suala ambalo linahusu taasisi, kama ana wafanyakazi ambao

wana malimbikizo hayo basi utaratibu upo kwa mujibu wa kisheria. Taasisi inayohusika itawasilisha kupitia ofisi ya Utumishi wa Umma na Wizara ya Fedha italipa fedha hizo kupitia *salary* ya *adjustment.* Kwa hivyo utaratibu upo kama wapo hao basi ufuatwe utaratibu na suala hilo litakamilika Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Nashukuru kwa majibu yake mazuri na taasisi inasikia, kwa hivyo, taratibu zitafuata ili wananchi waweze kupata haki zao. Tuendelee ahsante.

Kifungu PF0104	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Fedha na Mipango	76,985,837,000
	Jumla Kuu ya Fungu F01:	**154,764,013,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU F02 - MFUKO MKUU WA SERIKALI

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilioneshwa wasiwasi wangu sana na kifungu HF02010101 kufanya malipo ya matumizi maalum ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, nimesoma Katiba ya Zanzibar kifungu cha 35, 110 na kifungu cha 111 sikuona hata pamoja panaposema kufanya malipo ya matumizi mbali mbali na Mfuko huu wa Serikali umetajwa kikatiba kabisa. Lakini Mhe. Waziri wakati akiniambia alinambia hata pesa za maafa. Sasa mimi nilikuwa nina wasiwasi kwa sababu mwaka jana zilitengwa shilingi 38,951,000,000 lakini mwaka huu kuna pesa nyingi zaidi zimewekwa ni shilingi 45,460,580,000. Sasa nina wasiwasi kwa nini tusiorodheshewe au tukaambiwa kwa sababu hizi ni pesa za wananchi na pesa nyingi sana, haziwezi tu tukasema kufanya malipo au matumizi mbali mbali. Nilikuwa napata mashaka kidogo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Mohamed Said alionesha nia hiyo na nilijaribu kutoa ufafanuzi kwa hayo matumizi mengineyo katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Lakini nimhakikishie kwamba Katiba haiwezi kuweka wazi kila kitu, Katiba inazungumzia mafungu kwa ujumla, lakini kwenye matumizi ndiko kunakowekwa utaratibu mzima wa matumizi ambayo yatatumika katika mwaka wa fedha husika. Kwa hivyo akubaliane na mimi kwamba matumizi ya Mfumo Mkuu wa Serikali ni matumizi mengineyo yana matumizi mengi na nimezungumzia masuala ya matumizi maalumu ambayo yako kwa mujibu wa sheria nyengine, mafao ya viongozi, mishahara ya viongozi, safari, yako kwa mujibu wa sheria nyengine. Vile vile kuna matumizi ya dharura na suala la dharura hatulijui linakuja na *magnitude* gani, linaweza likaja suala dogo ambalo limo ndani ya bajeti, lakini linaweza likaja suala jengine kubwa nje ya uwezo Mfuko Mkuu wa Serikali ndio unaofanya shughuli hizo. Hakuna nchi ambayo inakuwa haina fedha za dharura za namna hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, fedha hizo kwa kuongezea zaidi huwa zinakaguliwa na taarifa yake inapatikana ya ukaguzi juu ya fedha na matumizi ya fedha nyenginezo.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nikimsikiliza vizuri sana Mhe. Waziri kaka yangu Dkt. Khalid Salum Mohamed na mtu ambaye namheshimu sana kwa kauli zake. Nimetizama vile vile Sheria ya Fedha ambayo wao wenyewe ndio wanayoitumia hakuna jambo hili, ningewaomba tu wanapoweka hapa matumizi haya tuweze kuarifiwa na tuweze kuona, kwa sababu unapoweka *bulk* kitu pamoja hujui kinaweza kikafanywa vipi na hizi pesa za wananchi. Mheshimiwa tuendelee.

Kifungu PF0201	Programu Kuu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali	134,035,300,000
	Jumla Kuu ya Fungu F02:	**134,035,300,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU F03 - TUME YA MIPANGO ZANZIBAR

Kifungu PF0301	Programu Kuu ya Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watenda kazi	1,624,500,000
Kifungu PF0302		

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia nilisikitishwa sana na utekelezaji wa miradi ya *PPP* hapa kwetu Zanzibar, lakini Mhe. Waziri nilikuwa nikimsikiliza vizuri sana wakati anatoa majibu. Mimi nilikuwa nataka maelezo ya kina kwa sababu alinambia kuna miradi tayari ime-*take off*, lakini ni miradi ipi ambayo ime-*take off*. Hapa nilikuwa nataka kuzungumza kisera zaidi sio kibajeti, aniambie ni miradi ipi ambayo ime-*take off* kwa sababu nina wasiwasi nayo na sheria yenyewe na nikasema sheria yenyewe hii inaweza kuwa ni sheria kandamizi serikali ifanyiwe *review* ili kuona basi sheria hii inaweza kuwa rafiki sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mohamed Said Mhe. Waziri alilitolea ufafanuzi suala hilo na alijibu, lakini Waheshimiwa Wajumbe Waziri anapotoa ufafanuzi juu ya hoja mara nyingi mnakuwa hampo au mnazungumza. Kwa hivyo Mhe. Waziri alilitolea Mhe. Mjumbe ufafanuzi, labda utwambie kuwa unataka ufafanuzi wa ziada lakini katika hilo pia hukuonesha nia ya kuzuia fungu. *(Makofi)*

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nikiandika moja baada ya moja majibu ya Mhe. Waziri akiyajibu tena alikuwa ananiona namsikiliza kwa makini sana na nilisema nataka ufafanuzi juu ya hili. Kama utakuwa tu mwenyewe una fedha yako au unabeba gunia la misumari endelea kubeba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee.

Kifungu PF0302	Programu Kuu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Takwimu	3,403,000,000
Kifungu PF0303	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Tume ya Mipango	1,793,900,000

Jumla Kuu ya Fungu F03: **9,430,837,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa sasa naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nami nichukue fursa hii kuwashukuru sana wachangiaji waliochangia, lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ambayo imewasilisha hotuba yake. Kwa hivyo, niwapongeze sana na nina imani Mhe. Waziri atayafanyia kazi yale yote ambayo wameyaleta katika hotuba hii. Kabla ya kuakhirisha naomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mwenyekiti Mohamed Said Mohamed wanatakiwa wakutane katika ukumbi wao wa bajeti.

Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa kazi zetu za leo ziliomo katika *order paper* yetu tumemaliza, sasa naomba niakhirishe kikao hiki mpaka kesho tarehe 14/06/2018 saa tatu asubuhi.

(Saa 6.50 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 14/06/2018 saa 3.00 Asubuhi)